SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## Chanzo cha vifo vya samaki Mto Mara chatajwa

UKURASA 4



## WASANII WATAKIWA KUZALISHA KAZI BORA

UKURASA 20

Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
Jumapili Machi 20, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580890
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Rais Samia afunga mjadala wa Lissu

**NI** kuhusu usalama wake atakaporejea, atoa maagizo makali matumizi fedha za serikali ... *Uk. 2*



# Mbowe apokewa kishujaa nyumbani

Umati wa wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakimlaki Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Freeman Mbowe (juu ya gari), alipowasili Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro jana, akielekea kijijini kwao, Nshara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Askofu Kilaini apongezwa kuhamasisha amani, upendo

UKURASA 4



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na mkewe Mama Mbonimpaye Mpango, wakikabidhi zawadi kwa Mhashamu Askofu Method Kilaini, baada ya kushiriki Ibada ya shukrani ya Jubilei ya dhahabu ya miaka 50 ya Upadre wa Askofu huyo, katika Kanisa Kuu Katoliki la Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera jana. **PICHA: OMR**

**MICHEZO** SIMBA YASAKA REKODI MPYA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ...Ataka kila senti itumike inavyopasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kila senti inayotolewa na serikali, itumike kwa kile ambacho imepangiwa kukifanya na si vinginevyo ili kuiwezesha nchi kuendelea kupiga hatua kimaendeleo.

Mkuu huyo wa nchi alitoa agizo hilo jana baada ya kupiga simu moja kwa moja kwenye kongamano la tathmini ya mwaka mmoja wa uongozi wake lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Alisema anawapongeza walioandaa kongamano hilo la tathmini ya mwaka mmoja wa uongozi wake na kuwataka Watanzania kuendelea kushikamana ili kujiletea maendeleo.

"Nimekuwa nikiwasikiliza toka mlipoanza kongamano lenu. Sikutegemea kama mambo yote ambayo mmeyataja hapa tumeweza kuyafanya katika kipindi hichi cha mwaka mmoja.

"Tumetoka mbali tunakokwenda ni mbali. Pia tutaweza kufika tu kama tutashirikiana, tutashikamana. Kila mmoja wetu awajibike katika nafasi yake. Kila senti inayopatikana, hata iwe ndogo itumike ipasavyo ili kufikia malengo yetu," alisema.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza katika kongamano hilo, alisema hadi Januari, mwaka huu, Rais Samia ametekeleza bajeti kwa kupeleka fedha katika maeneo mbalimbali kwa asilimia 60.5 ya bajeti yote.

"Kwa kipindi cha miezi sita tu toka Julai 2021 hadi Januari, 2022 ameweka rekodi ambayo haikuwapo hapo awali katika utekelezaji wa bajeti kwa kupeleka fedha katika maeneo yote kwa asilimia 60.5," alisema Dk. Tulia.

Alisema Rais ametekeleza kwa kishindo miradi ambayo iliachwa katika awamu ya tano na mtangulizi wake Dk. John Pombe Magufuli.

"Rais Samia katika kipindi hiki cha mwaka mmoja kwa lugha ya mtaani unaweza kusema ameupiga mwingi sana mama. Kazi inaendelea na mama Samia ameweza tena amepitiliza sekta ya afya imepata fedha hadi Januari, mwaka huu, asilimia 62.32, maji asilimia 76.51 TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) asilimia 39.32 na mikoa asilimia 56.03," alisema.

Dk.Tulia alisema Rais Samia alipoipokea nchi aliikuta katika changamoto kubwa ya ugonjwa wa UVIKO-19.

"Licha ya kuwa Mama Samia alichukua nchi katika kipindi cha majonzi baada ya kuondokewa na Rais Magufuli lakini alikutana na changamoto kubwa ya UVIKO-19 hali iliyomlazimu kutafuta fedha kutoka IMF trilioni 1.3 ambazo pia zimetusaidia kujenga madarasa na kuboresha miundombinu ya afya," alisisitiza

Alisema kuwa watu ambao walifikiri kuwa kutokana na kuwa mwanamke asingeweza lakini hadi sasa ndani ya mwaka mmoja tu amefanya makubwa na kuondoa dhana potofu iliyojengeka miongoni mwa watu.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akizungumza wakati wa kufungua kongamano la tathmini ya mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, lililofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia afunga mjadala kuhusu Lissu

**Na Thobias Mwanakatwe,** ARUSHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amevunja ukimya kuhusu suala la usalama wa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, huku akisema akirejea nchini ataishi kama Watanzania wengine wanavyoishi.

Amesema hoja ya kiongozi huyo kuhakikishiwa usalama pindi atakaporudi, haina mashiko kwa sababu kila mtu nchini ana usalama.

Rais Samia alitoa kauli hiyo juzi wakati akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusu mwaka mmoja wa uongozi wake tangu aingie madarakani baada ya kifo cha mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli. Magufuli alifariki dunia Machi 17, mwaka jana.

"Nimhakikishie usalama wake kwani ana wasiwasi gani? Kwani nani hana usalama ndani ya nchi? Sisi sote tumo humu ndani tuko salama. Akirudi ataishi kama Watanzania wengine wanavyoishi," alisema Rais Samia baada ya kuulizwa na mtangazaji kuhusu ombi la Lissu kuhakikishiwa usalama atakaporejea nchini.

Kauli hiyo ya Rais Samia imemaliza mzizi wa fitina juu ya maombi ya mara kwa mara ya Lissu ambaye kwa sasa anaishi nchini Ubelgiji. Lissu amekuwa akiitaka serikali impe hakikisho la usalama wake atakaporejea nchini.

Alipoulizwa kuwa wasiwasi wa Lissu kurejea nchini unatokana na watu waliomshambulia hawajapatikana na bado uchunguzi haujakamilika, Rais Samia alisema: "Uchunguzi wa tukio lake utakamilikaje wakati yeye hayupo? Inapaswa yeye arudi. Yeye ndiye mhusika, hivyo lazima awapo ili hao wanaofanya uchunguzi ashirikiane nao."

Kuhusu alipofanya mazungumzo na Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, baada ya kutoka gerezani kama kulikuwa na suala la kuombana radhi kwa yaliyotokea, alisema hakukuwa na suala kama hilo.

Hata hivyo, alisema walichozungumza ni kupiga mstari mwekundu matukio yaliyopita na kuyaweka kando na sasa jambo la msingi lililobaki ni kujenga nchi.

"Nani kamwomba radhi mwenzie? Hapa hakuna kuombana radhi. Tulizungumza kwamba tunapiga mstari mwekundu yaliyopita yamepita twende tukajenge nchi yetu," alisema.

Kuhusu kesi ya Mbowe kama itakuwa imetia doa utawala wake na kauli aliyowahi kuitoa wakati kesi ikiwa bado inaendelea mahakamani, Rais Samia alisema haijatia doa lolote wala kuleta ugumu kwa mahakimu na majaji kwa kuwa uongozi wake ni wa utawala wa sheria.

"Haikutoa wakati mgumu kwa sababu kile (mahakama) ni chombo pekee na ni mhimili unaofanya kazi kwa kujitegemea. Kwa hiyo nitakachosema mimi wala hakiwaathiri wao chochote. Mhimili wenyewe umekaa umefanya kazi zao basi," alisema Rais Samia.

# Mbowe apokewa kishujaa nyumbani

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), jana alipata mapokezi ya aina yake wilayani hapa ikiwa ni mara ya kwanza kufika baada ya kutoka gerezani hivi karibuni.

Kuwasili kwa kiongozi huyo wa chama kikuu cha upinzani nchini, kulisababisha baadhi ya shughuli kusimama kwa saa kadhaa huku mamia ya watu wakiwa wamesimama kando ya barabara wakimwangalia kila alipopita.

Mapokezi hayo yamemfanya aandike rekodi ya aina yake kisiasa na kuonyesha kuwa bado anaaminiwa na kuwa mwanasiasa wa upinzani mwenye haiba ya kupendwa. Pia ameonyesha mvuto wake katika harakati za kisiasa, bado unawavuta wengi kutafuta na kuiga ushawishi alio nao.

Kwa mapokezi ya jana, haijawahi kutokea katika wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, baada ya mamia ya wananchi wa Hai na viunga vyake, kujitokeza kumpokea. Mapokezi hayo yaliyohusisha pikipiki, magari madogo, mabasi madogo aina ya Toyota Hiace, Noah na Toyota Coaster kutoka miji ya Moshi, Siha, Hai na Arusha, yalianza safari kwenda Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) saa 3:00 asubuhi.

Mbowe wakati anaondoka uwanja wa ndege, msafara wake ulikuwa ukiongozwa na mbwa aliyekuwa ameshikiliwa na walinzi wake.

Alipofika katika makutano ya njiapanda ya KIA/Arusha/Moshi, Mbowe, ambaye alikuwa kwenye gari la wazi, aliwapungia wananchi na kuwashukuru, akitamka maneno haya, 'asanteni kwa kunipokea tuko pamoja'.

Katika mapokezi hayo, shughuli mbalimbali zilisimama kwa muda wakati msafara wa Mbowe ukitoka uwanjani KIA, kuelekea Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe, ambako wananchi walisimama kandokando ya barabara kumlaki, huku wakiwa wameshika majani ya 'sale' ambayo hutumiwa na kabila la Kichaga, kuonyesha amani au kuomba msamaha.

Baadaye saa 5:00 asubuhi, msafara wake uliondoka KIA na kwenda hadi mji mdogo wa Bomang'ombe ambako Mbowe alipumzika kwa muda katika ofisi yake ya zamani ya ubunge.

Saa 10:25 jioni, Mbowe na msafara wake waliondoka Bomang'ombe kwa msururu wa magari na pikipiki wakienda kijijini kwao Nshara, Machame ambako atakutana na ndugu, jamaa na marafiki kabla ya leo kwenda kutoa shukrani nyingine katika Usharika wa Nshara wa Jimbo la Hai la Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

TANGAZO



# PONGEZI

**BODI YA WAKURUGENZI, MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WOTE WA MAKAMPUNI YA IPP LIMITED TUNAKUPONGEZA SANA MHESHIMIWA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KWA MAFANIKIO MAKUBWA YANAYOONEKANA KWENYE NCHI YETU KATIKA KIPINDI CHA MWAKA MMOJA WA UTAWALA WAKO.**

**KAMPUNI ZETU ZITAENDELEA KUWA BEGA KWA BEGA NAWE KATIKA KUTIMIZA MAONO YAKO.**

***HONGERA SANA NA KAZI IENDELEE.***

IPP

# Waliokufa kwa ajali Morogoro wafikia 23

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

IDADI watu waliofariki dunia katika ajali iliyohusisha basi la Ahmeed lililokuwa likitokea Mbeya kwenda Tanga na lori katika eneo la Melela Kibaoni mkoani Morogoro, imeongezeka na kufikia 23.

Juzi, Ijumaa usiku idadi ya vifo vya ajali hiyo iliripotiwa kuwa 22 lakini hadi jana mchana majeruhi mmoja alifariki dunia hivyo kufanya idadi ya waliopoteza maisha kufikia 23 huku majeruhi watatu kati ya 26 waliolazwa wakipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa matibabu zaidi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Scholastica Ndonga, alisema majeruhi huyo alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu hospitalini hapo.

Ndonga alisema awali hospitali hiyo ilipokea majeruhi 37 na miili ya watu 13 wakiwamo wanaume saba na wanawake sita, na baadaye majeruhi zaidi waliokuwa katika hali mbaya walifariki dunia na kufikia vifo vya watu 23.

Ndonga alisema majeruhi watatu waliopata rufani kupelekwa Muhimbili kwa matibabu ni wanaume wawili na mwanamke mmoja.

Kuhusu utambuzi wa miili na majeruhi, Ndonga alisema bado kazi hiyo inaendelea ingawa juzi walikosa majina kamili ya baadhi ya majeruhi.

Baadhi ya majeruhi waliolazwa hospitalini hapo wakiwamo Mwanahawa Mbarouq , Bertha Aganila na Halfan Mwinchuma, walisema dereva wa lori alikuwa amelipita gari lingine na dereva wa basi walilokuwamo alijaribu kumkwepa lakini dereva wa lori akawa amerudi ghafla na magari hayo kugongana.

Kamishna wa Mafunzo na Opereshieni wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, aliwataka madereva kuchukua tahadhari wanapokuwa barabarani na kupongeza kituo cha ITV kupitia kipindi chake cha “Aibu Yako,” kupaza sauti kusaidia kukabiliana na makosa ya usalama barabarani.

Alisema madereva wote wawili waliohusika na ajali hiyo ambao bado hawajatambulika majina yao wamefariki dunia katika ajali hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shighela, alipongeza jitihada zilizochukuliwa za kuokoa majeruhi hususani kwa wauguzi na watoa huduma wa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro na Jeshi la Polisi.

Aidha aliwaonya madereva kutumia barabara kwa uangalifu na kuzingatia sheria za barabarani ili kuepuka ajali zinazoweza kuepukika.

“Hata kwenye hii ajali, inaonekana madereva wote walikuwa kwenye mwendo mkali, pia barabara hii inatumika hadi nchi za jirani hivyo ni vema kuwa makini wakiwa barabarani, “alisisitiza Shigella.

# Kilaini apongezwa kuhamasisha amani, upendo

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amempongeza Askofu Msaidizi wa kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba, Dk. Methodius Kilaini, kutokana na mchango wake wa kuhamasisha amani na upendo miongoni mwa Watanzania.

Akizungumza baada ya ibada ya Jubilee ya Miaka 50 ya Upadri wa Askofu Kilaini, iliyofanyika katika Kanisaa Kuu la Katoliki mjini Bukoba, Dk. Mpango alisema serikali inatambua na kushukuru kwa mchango wa kiongozi huyo wa kiroho katika Kanisa na kwa jamii ya Watanzania.

Dk. Mpango alimtaja Askofu Kilaini kuwa ni miongoni mwa waanzilishi wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini mwaka 1994 ambayo imeimarisha maelewano miongoni mwa waumini wa dini na madhehebu mbalimbali nchini.

Makamu wa Rais alilipongeza na kulishukuru Kanisa Katoliki kwa kuunga mkono juhudi za serikali kwa kutoa mchango mkubwa katika ustawi wa taifa kiroho, kiuchumi na kijamii.

“Kanisa limefikisha huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwemo yale ambayo serikali bado haijafikisha huduma hususani vijijini na maeneo wanakoishi watu wa hali ya chini mijini. Kwa kufanya hivyo, tunalipongeza kanisa kwa kuendelea kuhudumia yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu,” alisema Dk. Mpango aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika hafla hiyo.

Makamu wa Rais alisema serikali imejielekeza katika kuboresha na kujenga miundombinu ya usafiri na usafirishaji, elimu, afya na maji katika mkoa wa Kagera ili kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na uchimbaji wa madini kama mgodi wa Nikel Kabanga na kufungua fursa za biashara na ajira, hivyo kuwataka wananchi wa Kagera kutumia fursa hizo kukuza uchumi wao.

Pia aliliomba kanisa kufundisha na kulea vijana katika maadili mema na kuthamini kufanya kazi halali. Alisema katika nyakati hizi, kuna ongezeko la mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii ikiwamo ulevi, rushwa, uvivu, wizi na ufisadi, mauaji ya kutisha na idadi kubwa ya ndoa kuvunjika na kuongezeka kwa watoto wa mitaani. Askofu Kilaini kwa upande wake, aliishukuru serikali kwa ushirikiano iliompatia kwa kipindi chote cha miaka 50 ya utumishi wake.

Aidha, alimpongeza Rais Samia kwa mwaka mmoja wa uongozi wake wenye mafanikio makubwa na kazi nzuri alioifanya. Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia, taifa limeongozwa kwa utu, amani na mshikamano pamoja na hatua mbalimbali za maendeleo kwa wananchi.

Kilaini aliwashukuru wananchi wa mkoa wa Kagera kwa kuwa pamoja naye wakati wote wa utumishi wake na kuwaomba kuimarisha umoja, mshikamano, amani na kufanya kazi kwa bidii ili kuuletea maendeleo mkoa.




Balozi wa Biko Tanzania, Kajala Masanja (kushoto), akikabidhi fedha Sh. milioni 10 kwa Nuru Mikikadi (katikati), aliyeibuka mshindi wa droo kubwa ya Bahati Nasibu ya Biko, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Benki ya CRDB Tawi la Premier Palm Beach, Flamiana Msilu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chanzo cha vifo samaki Mto Mara chatajwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI maalum iliyoundwa kuchunguza mabadiliko ya maji katika Mto Mara na kusababisha samaki kufa, imekamilisha kazi hiyo huku ikibainisha kuwa chanzo ni kinyesi cha mifugo, shughuli za binadamu na nguvu za asili.

Maji ya mto huo yalibadilika rangi na kuwa meusi kisha kutoa harufu na kusababisha idadi kubwa ya samaki kufa, hivyo kumlazimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, kuunda kamati kuchunguza chanzo cha vifo hivyo.

Wajumbe wa kamati hiyo ni Dk. Kessy F. Kilulya, Mkuu wa Idara ya Kemia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Charles Kasanzu kutoka Idara ya Jiolojia UDSM, Daniel Ndio, Mkurugenzi wa Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali katika Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Renatus Shinhu, Mkurugenzi wa Bonde, Mamlaka ya Bonde la Maji Ziwa Victoria.

Wengine ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) Kituo cha Mwanza, Baraka Sekadende, Dk. Neduvoto Mollel kutoka Mamlaka ya Afya ya Mimea na Usimamizi wa Viatilifu (TPHPA), Ofisa kutoka Ofisi ya Rais Ikulu,

Yusuf Kuwaya kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara na Faraja Ngelageza, Mkurugenzi Msaidizi Bioanuai, kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais.

Akitoa matokeo ya uchunguzi mjini Musoma, Mwenyekiti wa Kamati, Profesa Samuel Manyele, alisema hali hiyo imetokana na kuwapo kwa kiwango kikubwa cha kinyesi cha mifugo pamoja na uozo wa mimea ndani ya mto hasa mimea vamizi kama vile magugu maji na matete. Prof. Manyele alisema hali hiyo ilisababisha kupungua kwa kiasi kikubwa kiwango cha oksijeni ndani ya mto, hivyo maji kubadilika rangi na kuwa na harufu mbaya, huku samaki wakikosa chakula na hatimaye kufa.

Hata hivyo, alikanusha picha zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilizokuwa zikionyesha samaki wakiwa wamekufa kwa wingi, akisema si kutoka Mto Mara.

HABARI KITAIFA

# Dereva jela miaka minne wizi mafuta

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Iringa, imemhukumu kifungo cha miaka minne jela na kulipa faini ya Sh. milioni 16 aliyekuwa dereva wa lori la mafuta la kampuni ya Panone, Faid Manis, baada ya kupatikana na hatia katika kesi ya jinai iliyokuwa ikimkabili yeye na wenzake sita.

Akisoma hukumu hiyo juzi, Hakimu Mkazi Mwandamizi Emmy Nsangalufu, alisema mahakama baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa mahakamani hapo pasipo shaka, imejiridhisha na kuwatia hatiani dereva huyo na wenzake watano kwa kosa la wizi wa kuaminika.

Washtakiwa waliofikishwa mahakamani hapo pamoja na Manis ni Abbas Finde maarufu kwa jina la Mchina, Frank Manjir, Gerald Mlelwa, Adam Mnzava, Leonard Mwambela na Gaspar Shirima.

Alisema washtakiwa hao walifikishwa mahakamani hapo kwa mashtaka matatu ya kula njama, shtaka la kwanza likihusisha wote saba, la pili ambalo lilimhusu dereva pekee ni wizi wa kuaminika wakati kosa la tatu lililowahusu washtakiwa namba mbili na saba ni wizi wa vitu vya kwenye gari zikiwemo lita 7,200 za mafuta .

Hakimu alisema kutokana na ushahidi uliowasilishwa, mahakama imemtia hatiani na kumfunga jela miaka miwili Manis kwa kosa la kwanza la kula njama na miaka miwili kwa kosa la pili la wizi wa kuaminika.

Sambamba na kifungo hicho, Hakimu Nsangalufu aliamuru dereva huyo kulipa fidia ya Sh. 16,050,000.

Wakati Manis akihukumiwa kifungo na kulipa faini, washtakiwa namba 2, 4 ,6 na 7 walikutwa na hatia ya kosa la kuiba vitu vya kwenye gari na kila mmoja kuhukumiwa kifungo cha miaka miwili na kulipa fidia ya Sh. 16,050,000 kutokana na wizi wa lita 7,200 za mafuta.

Hata hivyo, mahakama hiyo ilijiridhisha pasipo shaka yoyote na kuwaachia huru washtakiwa namba mbili na namba tano ambao ni Frank Manjir na Adam Mnzava.




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (katikati), akizindua chanzo cha hewa tiba 'Oxygen Generating Plant' chenye thamani ya Dola za Kimarekani 300,000 kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha mitungi ya oksijeni 200 hadi 250 kwa siku, kilichojengwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Korea Foundation for International Health Care (KOFIH), katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, mkoani Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Balozi wa Korea Kusini hapa nchini, Kim Sun Pyo na Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Prof. Lawrence Museru. **PICHA: CHRISTINA MWAKAKANGALE**

# RC aunga mkono uamuzi wa DC kuhamishwa stendi ya magari

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ameunga mkono uamuzi wa kuhamisha magari madogo ya abiria, maarufu kama Mchomoko, kutoka Stendi Kuu ya Mabasi ya Bariadi kwenda eneo la Soko Kuu.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji wa Bariadi lilipinga uamuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, la kuondolewa kwa daladala hizo, wakieleza ni wa kisiasa.

Katika kikao chao, madiwani hao walilalamikia uamuzi huo kwa madai kuwa umesababisha mapato ya halmashauri kushuka na ulifanywa na bila wao kushirikishwa. Akipigilia msumari kuhusu sakata hilo, Kafulila alisema serikali haikujenga stendi hiyo kwa ajili ya kuleta usumbufu kwa wananchi bali kwa ajili ya kusaidia wananchi wake.

Kafulila alisema kuwa msingi wa maamuzi yaliyofanywa kuhamisha magari hayo ni kupunguza usumbufu kwa wananchi.

"Uamuzi wa kuondoa magari madogo ulishafanyika na utabaki kuwa hivyo hivyo. Jambo la msingi kwa uamuzi huo ni kupunguza bughudha au usumbufu kwa wananchi. "Serikali ilijenga stendi hiyo kwa ajili ya kusaidia wananchi na msingi wa kuwapo kwa stendi hiyo ni wananchi watumie kwa mapenzi na si shuruti na hiyo ni azma ya serikali kuleta maendeleo kwa watu," alisema Kafulila.

Alisema suala la kupungua mapato watakaa na kuangalia namna bora ya stendi kuendelea kufanya vizuri ili kuweza kuongeza mapato ya halmashuari.

"Kwa kweli hatuwezi kukusanya mapato kwa ajili ya kusumbua watu, suala la mapato tutakaa tuangalie njia bora ya kuweza kuifanya stendi hiyo ifanye vizuri zaidi ya hapa," alisema Kafulila.

Akizungumzia mafaniko ya Mkoa wa Simiyu kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, alisema miradi yote ya maendeleo ambayo serikali imeleta fedha zake inaendelea kutekelezwa na itakamilika ndani ya muda uliopangwa. Kafulila alisema katika sekta ya maji, miradi yote 32 inayotekelezwa ndani ya mkoa huo pindi itakapokamilika itawezesha hali ya upatikanaji wa maji kwa kiwango cha asilimia 90 mjini na vijijini.

Kuhusu barabara, Kafulila alisema Mkoa wa Simiyu umetia saini mikataba 58 yenye thamani ya Sh. bilioni 11 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara za vijijini na mjini.

# Mloganzila kuanzisha benki ya maziwa

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, inatarajia kuanzisha huduma ya benki ya maziwa ya binadamu, yatakayohifadhiwa kwa ajili ya watoto waliozaliwa ambao mama zao wapo mahututi au kufariki.

Imesema hatua hiyo inatokana na majibu ya utafiti uliofanyika na kubaini kwamba inawezekana kuwa na benki hiyo.

Katika utafiti huo, asilimia 93 ya kinamama waliohojiwa ili kujitolea maziwa yao kwa watoto wasiokuwa wao, wameonyesha utayari wa kufanya hivyo.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji MNH, Dk. Julieth Magandi alitoa taarifa hiyo juzi mbele ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, baada ya kuzindua mtambo wa kuzalisha hewa tiba pamoja na huduma iliyoboreshwa ya Watoto Wachanga Mahututi (NICU).

Alisema mtambo huo ambao umegharimu Dola za Marekani 300,000, umeanza uzalishaji mwaka huu.

Dk. Magandi alisema mtambo huo pia una tangi la lita 4,000 lililojengwa na Taasisi kutoka Korea iitwayo Korea Foundation for International Health Care (KOFIH).

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto MNH-Mloganzila, Dk. Mwanaidi Amir, alisema benki hiyo inatokana na asilimia 60 ya wajawazito wanaojifungua hospitalini hapo kujifungua watoto njiti, huku baadhi ya mama zao wakiwa mahututi.

"Tuliona ni vizuri huduma hii iwepo ili mtoto apate ukuaji wa haraka tangu anapozaliwa kwa sababu maziwa ya mama baada ya kujifungua huwa na virutubisho vingi.

"Tutaangalia kinamama ambao wana maziwa mengi, ni kama mtu anavyochangia damu na utaratibu ni uleule, kupima magonjwa na kisha watachangia. Benki ya maziwa ambayo itaanza Agosti, siku ya unyonyeshaji duniani iwapo kila kitu kitakwenda sawa," alisema.

**UZALISHAJI GESI**

Alisema MNH-Mloganzila itaanza kuzalisha mitungi ya gesi 200 kwa siku na kuokoa Sh. mil. 33 kwa mwezi, zilizotumika kununua huduma hiyo kutoka kwa watu binafsi.

"Gharama ya kununua gesi kwa siku ilifikia mitungi 200 hadi 300, ambayo mmoja uliuzwa kati ya Sh. 20,000 na mkubwa ukiuzwa kwa Sh. 40,000. Mtaona namna serikali ilivyotumia fedha nyingi kwa ajili ya huduma hii muhimu kwa wagonjwa," alisema.

Kadhalika, Ummy alibainisha kukua kwa MNH-Mloganzila, sasa ni wakati wa kuanza kujitegemea kutoka chini ya usimamizi wa MNH tangu mwaka 2017, ilipokamilika ujenzi wake.

"Mloganzila ilikuwa inasimamiwa na Bodi ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, sasa itaanza kujisimamia kuanzia Julai, mwaka huu, kwa sababu kwa kipindi cha miaka mitano imefanya mambo mazuri," alisema.

Mbali na uzinduzi wa mtambo huo, Ummy pia alizindua jengo la huduma ya mama na mtoto lililoboreshwa, ikiwamo wodi ya watoto wachanga mahututi (NICU) walio chini ya siku 28, ambayo itahudumia watoto 60.

Balozi wa Korea Kusini nchini, Kim Sun Pyo alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika huduma mbalimbali za maendeleo ikiwamo za afya.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua kali zichukuliwe kudhibiti wimbi la ajali

**KATIKA** kipindi kisichozidi wiki moja, zimetokea ajali tatu za barabarani na kusababisha vifo vya watu 31 na wengine 98 kujeruhiwa. Ajali hizo zinahusu mabasi makubwa mawili ya abiria na madogo mawili aina ya Toyota Coaster na Toyota Hiace.

Katika ajali ya kwanza iliyotokea Machi 14, mwaka huu, katika eneo la Senjele mkoani Songwe, basi la Kilimanjaro Express lilipata ajali na kuungua vibaya huku watu wanne wakipoteza maisha na wengine 35 kujeruhiwa. Ajali hiyo ilifuatiwa na ile ya Coaster na Hiace katika kijiji cha Sindeni, Handeni mkoani Tanga ambayo ilisababisha watu wanne kufa papo hapo na wengine 37 kujeruhiwa.

Wakati tafakuri juu ya ajali hizo haijapotea katika fikra za watu, juzi ilitokea ajali ya basi la Ahmeed lililokuwa likitokea Mbeya kwenda Tanga baada ya kugongana na lori katika eneo la Melela Kibaoni mkoani Morogoro. Ajali hiyo ambayo chanzo chake ni lori lililokuwa likijaribu kulipita gari lingine, ilisababisha watu 23 kufariki dunia.

Kutokea kwa ajali hizo tatu ndani ya muda mfupi, kumeibua hisia tofauti miongoni mwa Watanzania ikiwamo udhibiti dhidi ya madereva wanaofanya makosa na utekelezaji wa sheria za usalama barabarani.

Ni ukweli usiopingika kwamba Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama barabarani linafanya kazi yake vizuri kuhakikisha wanaokiuka sheria wanachukuliwa hatua licha ya kwamba wako askari wachache wanaoendekeza rushwa ndogo ndogo kutoka kwa madereva wanaovunja sheria.

Hatua hiyo inathibitishwa na kile kilichofanywa na kikosi hicho baada ya kutokea kwa ajili ya basi la Kilimanjaro Express kwa mamlaka husika kumfutia leseni dereva aliyesababisha maafa hayo.

Kutokana na kuibuka kwa ajali hizo ambazo zimegharimu nguvu kazi ya taifa, ni vyema sasa hatua madhubuti zikachukuliwa kwa sababu mwenendo wa baadhi ya madereva wa mabasi ya mikoani katika utendaji kazi wao ni wa kutia shaka.

Tunasema hivyo kwa sababu katika safari kati ya Mbeya na Dar es Salaam, Arusha- Moshi hadi Dar es Salaam na ile ya mikoa ya kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi kupitia Dodoma hadi Dar es Salaam, kumekuwa na uendeshaji wa mwendokasi hali ambayo inaweza kusababisha ajali na kugharimu maisha ya watu.

Katika njia ya Dar hadi Mbeya kwa mfano, baadhi ya mabasi yamekuwa yakikimbia tofauti na miezi kadhaa iliyopita huku kukiwapo madai kwamba baadhi yameondoa vidhibiti mwendo vilivyowekwa. Baadhi ya madereva pia wamekuwa wakizidisha mwendokasi huku askari wa usalama barabarani wakiwasimamisha na 'kumalizana' nao kwa kuwashika mikono askari.

Licha ya kutokuchukuliwa hatua baadhi ya madereva, kumekuwa na msemo kwamba baadhi ya kampuni za mabasi yanayofanya safari katika maeneo mbalimbali, yamenunua njia, hivyo hayawezi kuchukuliwa hatua!


Ajali tatu zilizotokea ndani ya wiki moja, ziziamshe kutoka usingizini mamlaka zinazosimamia sekta ya uchukuzi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya wale wanaovunja na kikuika sheria za usalama barabarani.

Kama wahenga wasemavyo ukicheka na nyani, mwisho utavuna mabua, ni wakati mwafaka sasa kwa kikosi cha usalama barabarani na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuamka na kuwashughulikia wahusika ambao wanasababisha ajali na kugharimu maisha ya watu.

Kwa kufanya hivyo, ajali zinazotokana na makosa ya madereva pamoja na uzembe zinaweza kudhibitiwa.

Tanzania bila ajali inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii ichukue hatua, mmomonyoko wa maadili umejificha huku

Na Sabato Kasika

**KWA** kawaida, maadili mema ni seti yenye mambo yanayomwelekeza mtu katika jamii kutenda jinsi ambavyo inamjenga yeye mwenyewe na jamii kwa ujumla bila kusababisha migongano.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, maadili mema kwenye jamii ni msingi mzuri ambao kwa namna moja au nyingine humfanya mtu kuwa mwema na huwa yanafanana kutoka jamii moja kwenda nyingine.

Kutokana na hilo, binadamu tangu zamani wametoa miongozo maalumu ya maadili kulingana na dini, utamaduni, falsafa na kadhalika, kwa lengo la kuepusha mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii.

Mmomonyoko wa maadili unatafsiriwa kuwa hali ya kukiukwa maadili ya jamii fulani, na inawezekana ukasababisha kuwapo kwa vitendo ambavyo vinahatarisha maisha ya baadhi ya watu.

Hata katikati ya wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan amegusia tatizo la ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto kuwa ni kubwa nchini, na kwamba chanzo chake ni kuporomoko kwa maadili katika jamii.

Ni wakati akizungumza na watu wenye ulemavu Ikulu ya Chamwino, jijini Dodoma, anaonyesha kukerwa na jinsi ambavyo ndani ya jamii kuna mmomonyoko wa maadili unaosababisha vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Kutokana na hali hiyo, Rais anawataka wazazi na walezi kupaza sauti na kufichua wanaofanya vitendo hivyo ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale wanaojihusisha na kumomonyoa maadili.

Anabainisha kuwa tatizo linaanzia ndani ya familia na kuwataka watimize wajibu wao wa kusimamia maadili mema na kwamba tatizo hilo likifika ngazi ya taifa litakuwa limefanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na kupungua.

"Tatizo la ukatili wa kijinsia ni kubwa sana ndani ya nchi yetu na nilikuwa naongea na viongozi wa dini hapa kuna maporomoko ya maadili kwamba watu wameishiwa maadili, lakini kubwa ni kutomtambua Mungu. Rais anaendelea; "Kama unamtambua Mungu na unamjua Mungu unajua ndiyo aliyekutengeneza wewe amemtengeneza huyu huwezi kwenda na kufanya ukatili dhidi yake awe mzima au mwenye ulemavu," Rais Samia anasema.

> **"Kama unamtambua Mungu na unamjua Mungu unajua ndiyo aliyekutengeneza wewe amemtengeneza huyu huwezi kwenda na kufanya ukatili dhidi yake awe mzima au mwenye ulemavu," Rais Samia anasema.**

Kimsingi ni kwamba, malezi ambayo matokeo yake ni mtoto kuwa na madili mema, ni jukumu la kwanza la wazazi, ambalo hana budi kulitimiza kwa kushirikiana na jamii na tena kwa ustahimilivu mkubwa.

Bila malezi mema kwa watoto, ambao wanapitia hatua mbalimbali ukiwamo ujana ambao ni kipindi cha mabadiliko ya haraka katika mfumo mzima wa maisha, wanaweza kujikuta wasiwe na maadili mema kama wakiachwa.

Hivyo ingekuwa ni vyema kama kila mmoja wetu atakuwa makini katika malezi, kutokana na ukweli kwamba watu wanaishi katika mchanganyiko wakiwamo wasiojali hali ambayo inasababisha mmomonyoko wa maadili.

Umefika wakati sasa jamii kubadilika na kuzingatia kile ambacho Rais Samia ameagiza cha kurejea kwenye malezi yanayozingatia maadili mema ili kusiwepo mmomonyoko wa maadili unaochangia ukatili wa kijinsia.

Kutokana na mabadiliko makubwa kwenye nyanja mbalimbali ikiwamo ya elimu, afya, uchumi, mawasiliano, umbali kati ya wazazi na watoto unasababisha wakose malezi mema.

Ninaamini kwamba, ili watoto waweze kukomaa kiutu, wanahitaji kusaidiwa na wazazi na jamii ijitambue na kujifahamu ili kuwa wema kwani utu ndio msingi ambao juu yake unajenga maadili mema.

Kwa mantiki hiyo, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, ni vyema wasifumbie macho ukatili wa kijinsia ambao chimbuko lake ni mmomonyoko wa maadili, badala yake kila mmoja afanye sehemu yake kusimamia maadili mema.

Wazazi na walezi kukaa kimya bila kusimamia malezi mema ya watoto wao, inaweza kuwa sawa na kuhalalisha mmomonyoko wa madili, kuna haja ya kutafakari na kuchukua hatua sahihi ili kuwa na taifa bora la baadaye.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# KOSA KUBWA NISHATI KUTOKUWA KIPAUMBELE



Na Pascal Mayalla

KAMA kawaida, safu ya Kwa Maslahi ya Taifa, inaangazia mada anuwai kuhusu taifa letu la Tanzania, ikijikita kwenye mada za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kwa muda muda mrefu, safu hii imekuwa ikitokea kwenye makala magazetini na mitandao ya kijamii pekee. Kuanzia wiki hii, makala hizi pia zitaanza kuonekana kwenye luninga zetu katika kipindi cha TV kiitwacho "Kwa Maslahi ya Taifa". Kwa kuanzia, kitaanza kuonekana TBC na ITV na mambo yakienda vizuri, kitarushwa Star TV, Channel Ten na Azam TV, kwa lengo lile lile la kulisaidia taifa letu.

Si wengi wanafahamu kuwa ukiondoa uhai tuliopatiwa na Mwenyezi Mungu, hewa tuyayovuta na maji, kitu muhimu kuliko kitu kingine chochote ni nishati. Bila hewa, maji na nishati ya jua, hakuna mmea wowote unaoweza kuota, hivyo dunia inaweza kuangamizwa kwa baa la njaa. Mimi ni mmoja wa waumini wa falsafa ya maendeleo ya Mwalimu Nyerere, aliyoiandika kwenye kitabu chake cha "Binadamu na Maendeleo" kuwa ili tuendelee, tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora na kusisitiza kwamba "fedha si msingi bali ni matokeo tu. Tanzania, toka ile tunapata uhuru miaka ya 1960, vitu hivyo vyote vinne tunavyo. Sasa swali ni je, tunakwama wapi?

Japo mimi si mchumi, kwa maoni yangu, Tanzania tunakwama kwenye kupanga vipaumbele vyetu. Kwa muda mrefu, nchi wafadhili, mashirika ya kimataifa yanayotufadhili na yale ya misaada ya kimataifa, ndiyo yanatupangia vipaumbele vyetu ili kuwa katika nafasi ya kupata misaada ya kimaendeleo na mikopo yenye masharti.

Kwa vile sisi watu wa habari, si wachumi lakini kazi yetu ni kusikiliza tu wachumi na wakubwa wakipanga, hivyo kazi yetu ni kuripoti na kuandika kilichosemwa na wakubwa hawa, hivyo kujikuta, hatulisaidii taifa. Naamini kabisa kwa dhati ya moyo wangu kuwa Rais Samia ana nia thabiti ya kulisaidia taifa lakini ili afanikiwe ni lazima asaidiwe kuelezwa ukweli maeneo yenye udhaifu na yaliyotukwamisha ambayo ni eneo la upangaji vipaumbele vyetu. Moja ya maeneo hayo ni eneo nishati.

Kiukweli kabisa, licha ya Tanzania kugundua gesi asilia, kuwa na maporomoko ya Mto Rufiji, tuna jua la kutosha kuzalisha nishati ya jua (solar energy). Pia tuna upepo wa kutosha kufunga umeme utokanao na upepo (windmills) na chini ya ardhi tuna 'geothermal' ya kutosha kuzalisha umeme. Mpaka sasa ni nchi kubwa yenye watu milioni 60, lakini umeme wetu ni Megawati 1,600 tu. Tunapaswa kuruka badala ya kukimbia kuhakikisha tunapata nishati ya kutosha kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

.Japo tuna wataalamu na wataamuna, wachumi waliobobea, wanaopanga vipaumbele vyetu, kiukweli kwenye baadhi ya vipaumbele, wanazidi tu kumuingiza chaka Mama Samia. Namshauri Mama aendelee kuwasikiliza wataalamu wake wa uchumi, lakini pia asipuuze sauti zetu sisi kina yakhe. Kuna vitu tunaona tunakwenda ndivyo sivyo kwani tunashauri lakini tunapuuzwa. Nashauri pia tusikilizwe, huwezi jua tunaweza kusaidia. Vipaumbele vikuu vyetu vikuu ni elimu, kilimo, afya, nishati na miundombinu.

Wiki iliyopita katika siku ya 'Tanzania Day' kwenye Maonyesho ya Dubai (Dubai Expo 2020), Wizara ya Nishati ilifanya Kongamano la Kimataifa la Uwekezaji kwenye sekta hiyo ambalo lilihutubiwa na Waziri wa Nishati, January Makamba.

Baada ya kurejea nchini, nilimtafuta Makamba akasema: "Moja ya changamoto kubwa ya 'sub sector' (nishatri ndogo) ya umeme ni uwekezaji usiotosheleza. Nchi yenye ukubwa kama yetu, inayokuwa kwa kasi kama yetu na ongezeko la idadi ya watu kuwa na Megawati 1600 ni aibu kubwa. Au kuwa na mtandao mdogo wa usafirishaji umeme kama tulio nao ni aibu."

Mheshimiwa Waziri hakuishia hapo bali aliendelea kusema: "Tumezungumza na wawekezaji wengi, wakubwa wenye uwezo na nia njema ambao wako tayari kuja nchini kwetu na kuwekeza katika maeneo hayo."

Anasema kutokana na hali ya nishati nchini mwetu na fursa zilizopo Tanzania katika umeme, mafuta na gesi. Serikali, kwa mantiki hiyo, imedhamiria kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara ya nishati katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Makamba pia anasema Tanzania imedhamiria kufanya mapinduzi makubwa ya nishati kwa kuifanya nishati ya kupikia kupatikana kwa wingi na kwa urahisi zaidi kutokana na asilimia 70 ya nishati yote Tanzania kutumika kwa kupikia, ikifuatiwa na mafuta na umeme. Nishati kubwa inayoongoza kutumika kupikia ni nishati ya tungomotaka (biomass).

Makamba amesema ukweli mchungu kuwa: "Hali ya nishati nchini Tanzania si nzuri, watu 22,000 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na magojwa ya upumuaji yanayosababishwa na moshi wa kupikia kwa kuni na mkaa. Kutokana na hali hiyo, kipaumbele cha kwanza kwenye sekta ya nishati ni kuhakikisha gesi inapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu na inafika kwenye kila nyumba, hivyo kupunguza matumizi ya kuni na mkaa."

Pia Makamba amezungumzia hali ya nishati ya umeme nchini si nzuri kutokana na ukuaji mkubwa wa uchumi na ongezeko la idadi ya watu usiokwenda sambamba na uwekezaji kwenye sekta ya nishati, hivyo kinachofanyika sasa ni kutafuta fedha za kufanya uwekezaji mkubwa kwenye umeme ili kukidhi mahitaji.

Kwa upande wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Waziri Makamba anasema linahitaji transforma mpya zaidi ya 20,000 nchi nzima ili kuwa na umeme wa uhakika na kuacha kukatika mara kwa mara kutokana na zilizopo kulemewa. Kuhusu kukatikakatika kwa umeme, Waziri Makamba amesema kunachangiwa na ukuaji wa ghafla wa uchumi wa mtu mmoja mmoja hali iliyofanya watu wengi zaidi sasa kutumia vifaa vya umeme kulinganisha ilivyokuwa awali. Hali hiyo anasema imesababisha mahitaji makubwa ya matumizi ya umeme kwa wakati mmoja, kuongezeka maradufu na kusababisha kuyumbayumba kwa upatikianaji wa nishati hiyo.

Waziri Makamba anamalizia kwa kuwahakikishia Watanzania kuwa serikali ya sasa, chini ya Mama Samia, imedhamiria kwa dhati kukabiliana na changamoto zote zinazoikabili sekta ya nishati. Miradi ya kupeleka umeme vijijini iko pale pale na kwamba TANESCO iko kwenye mageuzi makubwa ya kiutendaji kuboresha huduma zake.

Anasisitiza kuwa shida zilizopo tunazijua, changamoto tunazijua, majawabu tunayajua, hivyo kinachohitaji ni subra na uvumilivu na baada ya muda si mrefu, kukatika katika umeme, kutakuwa historia.

**Wasalaam +255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Chifu Hangaya madonda yanauma kwa mbaaali!



Na Joseph Kulangwa

**Ni kama alivyolia siku anateuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Magufuli, bila shaka siku anatangaza kifo cha JPM hakulia tu kumpoteza bosi wake wa karibu bali pia majukumu yaliyokuwa mbele yake kama kiongozi wa nchi.**

IPO simulizi kuhusu mtoto na chupa ya chai. Iko hivi. Mama alikuwa na mwanawe akimpenda sana. Ili kuhakikisha anapata chakula chake kwa wakati na joto mwafaka, alimnunulia chupa kwa ajili ya uji.

Aliinunua kwa bei ambayo kwa maisha yake ilimtikisa kidogo, hivyo akawa makini sana, kuangalia haivunjiki na kulazimika kununua nyingine, kwani alijua hali yake kifedha ilivyokuwa. Hiyo ilimlazimu kuwa makini.

Kuna siku moja , mwanawe aliisukuma ikaanguka lakini Mungu saidia haikupata madhara. Lakini mama akaona ni vyema akawa mlinzi madhubuti wa chupa, hivyo kila alipomwona mwanawe akiisogelea akawa mkali.

Ulifika wakati akimbaraza mabao alipoigusa, akichelea kuivunja. Hivyo kwa mwanawe chupa ile haikuwa tena faraja bali iligeuka mateso kwani ilichangia sana kumsababishia maumivu kutoka kwa mamaye.

Kwa kulielewa hilo, mtoto huyo akaona hata bila chupa ile kuwapo uji kwake ni mahitaji ya msingi na mama asingeweza kuvumilia kumwona akilia njaa na kumkosesha uji, eti kwa sababu chupa haipo.

Hilo alilielewa vizuri sana mtoto yule, hivyo akapata wazo la kuihujumu ile chupa kwa kuibamiza ili isambaratike na mateso yake yaishe, akijua tu kuwa baada ya hatua hiyo, angeadhibiwa lakini kwa muda na baadaye mateso yangetoweka.

Kweli, siku moja mamaye hayupo kaenda kuganga njaa, akaibamiza chupa ile ikavunjikilia mbali na yeye akajiandaa kisaikolojia kupata kibano cha mama atakaporejea. Ndivyo ilivyokuwa, alikula kisago cha mbwa koko lakini mateso ya kufokewa na kuchapwa kwa ajili ya chupa yakawa yamekwisha.

Kwa nini nimeikumbuka hii simulizi? Ni kutokana na tathmini ya mwaka mmoja wa Chifu Hangaya madarakani. Jana ndiyo siku aliyokamilisha mwaka tangu atwae hatamu kutoka kwa mtangulizi wake, Hayati John Magufuli.

Kama alivyopata kusema, Chifu Hangaya aliingia madarakani kwa kudra za Mwenyezi Mungu. Bila shaka mawazoni mwake hakufikiria siku moja aje kuwa kiongozi mkuu wa nchi na bila shaka hata siku ile anatoa taarifa ya kifo cha JPM, hakuwa anaamini kwamba zamu ya kuongoza nchi imemfikia.

Ni kama alivyolia siku anateuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa Magufuli, bila shaka siku anatangaza kifo cha JPM hakulia tu kumpoteza bosi wake wa karibu bali pia majukumu yaliyokuwa mbele yake kama kiongozi wa nchi.

Lakini alipoingia akaapa, akaahidi kuitumikia nchi na watu wake kwa moyo na dhamira ya dhati na kweli, hakuna asiye shuhuda wa haya anayoyafanya Chifu Hangaya. Kama alivyoahidi kuponya madonda, tunaona, hivi sasa yanauma kwa mbaali!

Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Awamu ya Sita, kama wasemavyo anaupiga mwingi kwa kweli. Nchi imetulia, anakwenda taratibu lakini kwa uhakika. Alishasema yeye hatagombana na watu hadharani kwa kuvunja chupa ya chai.

Anajua madhara ya kufokeana fokeana hadharani majukwaani. Akasema yeye yake ni kalamu tu. Ukimzingua mnazinguana tu. Ukiharibu utaiona rangi yake lakini kimyakimya. Hata siku moja kumwona jukwaani akiuliza nimfanye nini huyu! Asilani!

Angalia anavyokutana na makundi ya watu, wa dini, wa siasa, wanawake, vijana, wenye ulemavu na wengineo, huko kote anatafuta kusikia ni jinsi gani Tanzania iwe na kila mtu afurahi kuwa Tanzania na kuwa Mtanzania.

Chifu Hangaya pamoja na uchifu wake wa taifa, anaishi kama mama na wanawe. Haangalii huyu ni mweupe huyu mweusi, yule mrefu na huyu mfupi, huyu mnene na yule mwembamba. Wote ni wanawe na anawahudumia sawa.

Katika kauli zake hatujasikia katika mwaka huu mmoja akisema kwa wapinzani hatupeleki maendeleo. Angalia hiyo trilioni 1.3 ya IMF ilivyosambaa nchi nzima na kufanya maendeleo hata waliko wapinzani.

Ni pesa kidogo sana lakini imemgusa karibu kila Mtanzania. Huko nyuma zilikwenda wapi? Chifu Hangaya upige hivyo hivyo Mama, tuko nyuma yako. Tanzania ni yetu sote.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Waziri Ndumbaro anastahili pongezi mikakati ya kutangaza utalii kimataifa



Na Thobias Mwanakatwe

TANZANIA ni miongoni mwa nchi duniani zilizojaliwa kuwa na idadi kubwa ya vivutio vya utalii kuanzia maeneo ya kihistoria.

Kwa uchache tu, Hifadhi za Taifa ambazo zimekuwa kimbilio kubwa la watalii kutoka nje ni pamoja Manyara, Serengeti, Mikumi, Seleous, Ngorongoro na zingine nyingi wanyama na ndege wa aina mbalimbali.

Pia iko milima kama vile Meru, Oldonyo Lengai wenye volkano na Kilimanjaro ambao ni mrefu kuliko yote barani Afrika. Kadhalika, kuna Kreta ya Ngorongoro na Bonde la Olduvai linalosemekana kuwa ni chimbuko la binadamu wa kwanza. Hivyo ni baadhi tu ya vivutio vilivyopo nchini.

Pamoja na Tanzania kubahatika kuwa na vivutio vingi na vizuri, kumekuwa na malalamiko mengi kuwa idadi ya watalii wanaovitembelea ni wachache kulinganisha na nchi jirani kama Kenya.

Lakini pia kwa muda mrefu Watanzania wamekuwa wakilalamika kuwa wenzetu wa nchi jirani wamekuwa wakitumia baadhi ya vivutio vilivyopo nchini kama vile Mlima Kilimanjaro kwa kuutangaza kimataifa kwamba uko katika nchi yao.

Kutokana na propaganda hiyo, watalii wamekuwa wakimiminika kwa ajili ya kwenda kuungalia lakini cha ajabu wakifika huko wanaletwa Tanzania ambako ndiko mlima huo mrefu barani Afrika unapatikana. Ni jambo lililowazi kuwa propaganda hizo zilizokuwa zikitumiwa na majira zetu, ziliinufaisha nchi yao kupitia vivutio vilivyopo Tanzania.

Kilio kingine cha Watanzania wakiwamo wabunge ni kwamba pamoja na Tanzania kuwa na vivutio vingi, havitembelewi na watalii wengi wa kutoka ndani na nje ya nchi kwa sababu havitangazwi na mamlaka zinazohusika.

Tatizo la kutovitangaza vivutio vya utalii vya hapa nchini kimataifa kwa kiwango cha juu ambalo limekuwa la muda mrefu kwa sasa, kwa mtazamo wangu, naona limeanza kupatiwa ufumbuzi na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Nayasema hayo hasa kutokana na juhudi kubwa na za wazi zinazofanywa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ambaye hivi sasa anajitahidi kutembelea nchi mbalimbali duniani kwa ajili kuvipigia debe vivutio vya utalii vya hapa nchini.

Nilisoma katika mtandao mmoja wa kijamii baadhi ya watu wakidai anachokifanya waziri Ndumbaro siyo sahihi kwani kazi ya kuvitangaza vivutio vya utalii haikupaswa kufanya na waziri kwani ipo idara inayohusika na mambo hayo.

Nilishangaa hoja mfu hizo ambazo hazina maana na haya mambo ya kusema bosi asifanye kazi fulani eti kwa sababu yupo mtu fulani anayepaswa kuifanya kazi husika ndio yanatuchelewesha kimaendeleo.

Nikuombe Waziri Dk. Ndumbaro endelea kuchapa kazi na kama ikiwezekana tembelea nchi zote duniani kwa ajili ya kutangaza vivutio vyetu hizi kelele za kusema ungeziachia idara zilizopo chini yako ndizo zifanye kazi hiyo achana na mawazo hayo.

Mimi binafsi nasema kimsingi nimevutiwa sana na mikakati hii ya Dk.Ndumbaro ambayo nadiriki kusema waliomtangulia katika wizara hiyo japo walifanya kwa kiasi chao lakini sio kwa kiwango cha juu kama anavyofanya waziri huyu makini.

Katika kipindi cha ndani ya mwezi huu nimekuwa nikimfuatilia Waziri Ndumbaro kwenye vyombo vya habari ambapo amefanya mazungumzo na uongozi wa klabu ya soka ya Ajax ya Uholanzi ili itangaze vivutio vya Utalii vya Tanzania kupitia matangazo ya jezi na mbao za matangazo (billboards) uwanjani.

Hakuishia hapo Dk. Ndumbaro ametembelea na kufanya mazungumzo na uongozi wa klabu kubwa ya Golf nchini Uholanzi ya GC BurgGolf Westerpark, Zoetermeer.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk.Ndumbaro pia amefanya mazungumzo na uongozi wa vilabu vya Atletico Madrid na Getafe vinavyoshiriki ligi kuu nchini Hispania (Laliga) kwa lengo la kuitangaza Tanzania katika sekta ya utalii.

Dk. Ndumbaro amefanya mazungumzo na klabu ya Real Valladolid inayomilikiwa na mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Brazil, Ronaldo De Lima, ikiwa ni jitihada za kuutangaza utalii wa Tanzania.

Pia hivi karibuni, Waziri Ndumbaro amefanya mazungumzo na uongozi wa juu wa Shirika la Ndege la Umoja wa Falme za Kiarabu (Emirates) kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania. Kwa mpango huo, vivutio hivyo vitaweza kuonwa na abiria wapatao milioni 90.2 wanaosafiri kila mwaka kupitia ndege za shirika hilo.

Aidha, tangazo la vivutio vya utalii vya Tanzania litakuwa likitazamwa na mamilioni ya abiria wa shirika hilo wakati ndege zitakapokuwa zikiruka katika viwanja mbalimbali duniani. Katika mazungumzo hayo wamekubaliana ziandaliwe makala tano (documentaries) za kuelezea vivutio vya utalii vya Tanzania zikiwamo Zanzibar, Serengeti, Ngorongoro na Mlima Kilimanjaro.

Mikakati hii inayofanywa na Dk. Ndumbaro hakika inafaa kuigwa na mawaziri wengine kwani mambo anayoyafanya yataiinua sana sekta ya utalii kimataifa. Kila mmoja anafahamu kuwa Tanzania inategemea utalii wa wanyamapori kwa asilimia 100, hivyo kupitia mkakati huu wa kutangaza vivutio vingine vya utalii kama vile utalii wa fukwe, utalii wa utamaduni na wa ikolojia, kutawezesha utalii huo kujulikana duniani kote.


Niwasihi tu idara nyingine zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kumuunga mkono Dk. Ndumbaro ili mipango yake hii ifanikiwe kwa kiwango kikubwa, hivyo kuifanya sekta ya utalii Tanzania kupaa kimataifa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia baruapepe mwanakatwe2005@yahoo.com au 0692-276999**

## DARASA LA NDOA

# NINI MAANA YA UPENDO WA DHATI KATIKA NDOA?



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KAMA inavyojulikana, ndoa ni taasisi kongwe na ya kwanza ya kijamii ambayo Mungu aliianzisha duniani. Taasisi hii ili idumu inahitaji malezi ya mume na mke na ili ikue na kudumu hatimaye kuwa na furaha ni lazima uwapo upendo wa dhati.

Upendo hauji kimiujiza bali hutengenezwa kwa matendo na kauli njema za mwenzi. Kwa mantiki hiyo, ni muhimu kila mwanandoa kuangalia mambo anayomtendea na kumnenea mwenzi wake.

Swali la msingi la kujiuliza ni je, kauli na matendo yako kwa mwenzi wako ni baraka au karaha?

Mwanandoa mwenye upendo wa dhati atamtendea na kumnenea mambo mema mwenzi wake. Upendo ni kutenda wema na kunena mema juu ya binadamu mwingine. Mwanandoa mwenye kutenda wema, hukataa roho ya ubinafsi na kiburi na hutanguliza mahitaji na kujali hisia za mwenzi wake.

Penye upendo wa dhati pana kujengana, kuimarishana, kushirikiana, kusaidiana, kutunzana, kuchukuliana, kuheshimiana, na kusameheana ili kufikia malengo na mafanikio ya ndoa.

Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri na kuonyesha moyo wa uvumilivu kwani ubora wa mwenzi hubebwa na kasoro za mwenzi wake. Hii ina maana kuwa mwanandoa huongeza thamani na kuonyesha ubora wake pale anapofanikiwa kumsaidia mwenzi wake katika udhaifu alio nao.

Mwenzi mwenye upendo wa dhati hushauri bila kuchoka na kumwomba Mungu ili ashughulike na udhaifu wa mwenzi wake.

Upendo wa dhati ni kizuizi cha hasira na uamuzi hatarishi, humsukuma mwanandoa kufikiri athari za hasira na maamuzi yake juu ya mwenzi wake. Pia huleta utu katika hushughulika na migogoro.

Hauweki vinyongo na kumbukumbu za makosa wala kulipiza visasi, bali humsukuma mtu katika kusamehe makosa na kuendeleza maisha.

Aidha, upendo wa dhati huvutia tabia ya kupenda kusema ukweli kwa kuwa ukweli hutuweka huru na udhalimu. Ukweli ni chimbuko la haki katika maisha.

Pamoja kwamba ukweli unauma, ni dawa ya nafsi iliyojeruhiwa na yenye kutamani mambo mema.

Hivyo, wanandoa wajifunze na kupenda kuelezana ukweli kuhusu maisha na matamanio yao. Kuweka mambo moyoni hakuleti tija bali hubomoa afya na maisha.

Siku zote upendo wa dhati huleta ulinzi (protects). Humsaidia mwenzi kujisikia yuko salama katika uhusiano wake wa ndoa; humlinda dhidi ya vitendo vya ukatili na kuleta msukumo wa kutenda mema.

Upendo wa dhati husimika uhusiano wa wanandoa na kuwafanya kuwa wamoja zaidi.

Dhana nyingine ni kwamba upendo wa dhati huleta tumaini (trust) na uhai wa ndoa. Wanandoa wanaopendana huaminiana.

Kutokuaminiana katika ndoa huleta hofu na shaka ambayo humwondolea mwenzi hali ya kujiamini.

Chochote kinachopita mbele yake ataona anaibwa au anasemwa yeye. Maisha yenye hofu na shaka husababisha utumwa na hudhoofisha afya ya mwili na akili.

Upendo wa dhati huleta matumaini (hopes) kuhusu maisha. Siku zote upendo huu huleta msukumo kwa mwenzi wa kuona mbele zaidi au mema yajayo.

Kuruhusu fikra zetu kuona mambo katika mtazamo chanya ni mwanzo wa kuruhusu maisha yenye ushindi na mafanikio ndani yetu.

Wanandoa wanapokuwa na mtazamo chanya kuhusu maisha yao wanakuwa wamechagua amani na furaha kuingia ndani yao.

Maisha ni pamoja na utamu na uchungu, hivyo upendo wa dhati haushindwi na lolote hata pale yanapotokea mabadiliko katika maisha.

Mwanandoa mwenye upendo wa dhati huwa hakimbii matatizo, bali humtia moyo na kumfariji mwenzi wake wakati wa huzuni na changamoto.

Kila ndoa hupitia hatua mbalimbali za maisha. Hatua hizo na mabadiliko yanayotokea ndio yaletayo changamoto. Kila ndoa nzuri imepitia changamoto.

Kwa hiyo, wanandoa wawe tayari kuzikabili changamoto na kuyapokea mabadiliko. Upendo wa dhati wa mwenzi huonekana na kuthibitishwa wakati wa changamoto.

Uwapo wa mwenzi uonekane katika raha na shida. Ndoa zilizodumu na zenye furaha ni zile ambazo changamoto zilipotokea, wanandoa walizikabili kwa pamoja.

**■Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

MACHI 20, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 13

**MITINDO YA NYWELE**
**Inayowapagawisha wanaume**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA
Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo




Ukurasa 12




# NGUVU YA YAI
# hung'arisha ngozi, huondoa madoa

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | S | A | U | M | U |
| | U | | | I | |
| T | B | C | | H | |
| | I | | T | O | A |
| | R | | | G | |
| D | A | M | P | O | |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
VUA, KOO, KOMBA, MKATE, TIBUKA, MSONDO

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

TUMIA RANGI YA NJANO, BLUU NA NYEKUNDU KUPAKA MCHORO HUU!



## CHEKA

Alichokifanya daktari

MAMA alikuwa anafanya usafi chumbani kwa mtoto wake, mara akaona mfuko chini ya uvungu wa kitanda. Alipokifungua akakuta kuna mawe madogo madogo ndipo alipomuita mtoto wake na kuanza kumhoji.

**Mama:** Mfuko huu wenye mawe wa nini?

**Mtoto**: Mama nisamehe

**Mama:** Nikusamehe nini wakati sijui haya mawe unayafanyia nini?

Mtoto: Huwa kila siku naingia bandani naiba mayai na hayo mawe ni idadi ya mayai niliyochukua.

**Mama:** Tuseme ndo umeiba haya yote? We kweli hunionei huruma

**Mtoto:** Mawe mengine niliyatupa baada ya mfuko kujaa

Mama: Tobaaa

**SWALI**

Mto Maragalasi unapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Je, unamjua rafiki yako mzuri ni yupi

***KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilichambua sifa za marafiki bora ambao unapaswa kuambatana nao ili ufanikiwe.***

Nikasema si kila rafiki ni wa kusogeza karibu. Si kila mtu wa kupeleka nyumbani kwako, hapana. Wengine hawafai. Si kila mtu anatakiwa kuwa rafiki yako.

Wapo marafiki ambao kazi yao ni kusengenya wenzao.

Kwa ujumla, rafiki mwema ni yule mwenye hofu ya Mungu. Mwingine ni rafiki anayekutia moyo wakati wote. Pia nikasema rafiki bora hukudokeza siri ya mafanikio yake. Rafiki wa aina hii ni wachache sana kwani wengi wetu hatupendi wengine wajue tulivyofanya mpaka kufanikiwa.

Ni vema kuwa rafiki na mtu anayeona mbele, atakayekusaidia na kukupa mawazo mazuri ya biashara na zaidi sana, mtu anayemtafuta Mungu kwa bidii.

Mungu anasema hivi katika moja ya neno lake kwamba, "Nawapenda wanipendao na wanitafutao kwa bidii watanione". Kumbe tukimtafuta Mungu kwa bidii, naye atatufanikisha katika kila jambo tutakalo kulifanya.

Mpenzi msomaji, hebu sasa nimalizie kukupa sifa mbili zaidi za rafiki aliye bora kwa mafanikio yako. Rafiki mwema hukufaa wakati wa jua. Wakati wa mafanikio rafiki zako watakutambua na wakati wa shida zako utawatambua marafiki zako. Maisha Ndivyo Yalivyo!

Hakuna mtu asiyepitia vipindi vigumu katika maisha. Kuna kupanda na kushuka, kuna kutembea na kuanguka! Katika nyakati ngumu ndipo unapohitaji msaada wa Mungu kupitia kwa marafiki zako.

Ukifilisika wale uliokuwa ukila na kunywa nao baadhi hutoweka, wanaobaki ni wachache sana. Neno la Mungu linathibitisha pale linaposema;- "Ndugu wote wa maskini humchukia; Jinsi gani rafiki zake huzidi kujitenga naye! Huwafuata kwa maneno, lakini wametoweka".

Hata watu wa nyumbani mwako watakuchukia na kukukwepa unapopata shida. Kuna baadhi ya familia hujitenga na ndugu mwenye ugonjwa au ukata muda mrefu. Huonekana kuwa ni mzigo.

Namkumbuka baba mmoja aliyepata ajali ya kuangukiwa na gari na kupooza miguu yote. Mke wake kuona vile akamkimbia na kwenda kuolewa na mwanaume mwingine.

Mfano mwingine mzuri wa rafiki anayekukimbia wakati wa jua ni ule wa mwana mpotevu. Alipopewa urithi na baba yake alisafiri kwenda nchi ya mbali. Huko alishirikiana na marafiki wabaya na baada ya kufilisika wote wakamkimbia, akaenda kufanya kazi ya kulisha nguruwe.

Sifa nyingine ya rafiki mwema, hukutetea wakati wote. Kuna marafiki au ndugu wa mchana lakini usiku hukuchoma. Hakuna mtu aliye mkamilifu katika mambo yote, na walio wa kwanza kuona mapungufu yako ni wale walio karibu na wewe!

Msomaji wangu, imekuwa ni kawaida kwa wale walio marafiki wanapopeana migongo tu, huanza kuanika madhaifu ya mwenzake. Hivi kulikuwa na ulazima wa kufanya hivyo? Je, mtu wa aina hii anamtakia mema mwenzake?

Akikuta watu wanamchambua rafiki yake, badala ya kumtetea, hujiunga nao kumsema na kugeuka kuwa rafiki 'mtaabishaji' kama wale marafiki wa Ayubu!

Kitu ambacho mtu anapaswa kujihadhari nacho ni kujiepusha na marafiki wanafiki. Lipo andiko la Mungu linasema; "Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake ". Sote tunapaswa kujiuliza, je, tupo tayari kuutoa uhai kwa ajili ya wengine?

Bila shaka msomaji wangu umejifunza mengi kuhusu aina za marafiki unaopaswa kuwa nao ili mambo yako yaende vema. Ukizingatia hayo na mengine nitakayoendelea kukujuza katika safu hii kadiri muda unavyoruhusu, naamini kabisa kwamba utaona nuru njema katika maisha yako!

Kwa leo niishie hapa lakini kwa neema ya Mungu wiki ijayo baada ya kuchambua aina za marafiki, tutaangalia umuhimu wa kuwa na marafiki au washirika katika kufikia hatma ya maisha yako.

Hakika, Maisha Ndivyo Yalivyo. Je, unayo maoni, ushauri au kisa chochote cha kimaisha ambacho ungependa tukijadili kwenye safu yetu hii? Tuma ujumbe mfupi kupitia namba 0715268581.

***Msomaji, bila shaka umefurahia shuhuda hizi kuhusu nafasi ambayo Mungu ameweka mbele yako kwa maisha yako. Je, una maoni,kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Mwaka mmoja wa Samia tuyaone matamanio mazuri

NI mwaka mmoja tangu Rais Samia Suluhu alipoingia madarakani kuongoza nchi akiwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo nchini na Afrika Mashariki. Hadi sasa ameonyesha anaweza, hivyo kuondoa imani hasi kuwa mwanamke hawezi kuaminiwa katika nafasi kubwa.

Wanawake wa Tanzania na Afrika tunatembea kifua mbele kwa kuwa tuna mfano wa kuwaonyesha mabinti zetu kuwa inawezekana ili wasikubali kikwazo chochote kinachoibuka kutaka kuzima ndoto zao.

Tangu kuingia madarakani kumekuwa na mabadiliko makubwa hasa ya kidemokrasia na kuondoa malalamiko ya kuminywa kwenye uhuru wa kujieleza na wa vyombo vya habari nchini.

Kwa haraka, Rais aliagiza kufunguliwa kwa vyombo vya habari vilivyokuwa vimefungiwa na tayari vimeshafunguliwa huku Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, akitangaza kutia saini marekebisho ya kanuni za mtandaoni na kukaribisha wadau kupeleka maoni ya Sheria ya Huduma za Habari.

Tunampongeza Rais Samia kwa kazi nzuri ya kuwaunganisha Watanzania na kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Tunamuunga mkono kwa kazi nzuri anayoifanya na tunaahidi kuendelea kushiriki ujenzi wa taifa.

Mara kadhaa Rais Samia amewataka Watanzania kushiriki ujenzi wa taifa imara, kwamba ni matamanio yake kila mmoja ashiriki kujenga nchi, kwa maana ya kwamba ni wajibu wa kila Mtanzania kuhakikisha nchi yake inafanikiwa katika nyanja nyingi.

Wajibu mkuu wa serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa watu wake kutekeleza majukumu yao na kwamba ihakikishe sekta binafsi inashamiri na kuajiri watu wengi, huku ikichangia maendeleo ya nchi, kwa kuwa ni kweli kwamba serikali haiwezi kuajiri wote wenye sifa ya kuajiriwa.

Tangu kuingia madarakani, tumeona mabadiliko makubwa kwenye sekta mbalimbali, huku mzunguko wa fedha mtaani ukirudi na sekta binafsi ikianza kurudi kwenye mstari baada ya kusinyaa kwa muda mrefu kutokana na mazingira magumu ya kufanya biashara.

Uhusiano wa kimataifa umeendelea kuimarika kwa nchi na sasa wadau na maendeleo wanamiminika nchini, hali iliyoongeza nafasi ya Tanzania duniani ikiwamo kuendelea kuaminiwa na mashirika makubwa ulimwenguni ushahidi tunaouona kwenye mikopo tunayopata.

Ndani ya kipindi chake cha uongozi, wanafunzi wote waliofaulu darasa la saba wameendelea na kidato cha kwanza kutokana na uwepo wa vyumba vya madarasa vya kutosha tofauti na miaka mingine iliwalazimu kuingia kwa awamu kwa kuwa miundombinu haitoshi.

Haya ni mafanikio yanayopaswa kuungwa mkono,kwa kila mtanzania kuwajibika ipasavyo katika eneo lake kwa kufanya kazi kwa bidii.

Tayari imeundwa kamati kupitia sheria na kuangalia namna bora kwa vyama vya siasa kufanya mikutano bila usumbufu ili kuwe na uwanja sawa wa kufanya siasa,jambo ambalo ni jema sana kwa manufaa ya nchi kwa kuwa kumekuwa na mvuto mkubwa.

Ni muhimu kuhakikisha mazidhiano yanakuwepo ili kuwa na uwanja wa siasa safi kwa manufaa ya watanzania,kuondoa mgawanyiko au mpasuko kwa kuwa mara zote rais ameonyesha nia njema ya kuwaunganisha watanzania wajivunie nchi yao.

Mjenga nchi ni mwananchi na mbomoa nchi ni mwananchi. Pia tuna wajibu wa msingi lakini kwa viongozi wanaomsadia Rais, wanao wajibu vile vile wa kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zinafuatwa kikamilifu.

Bado tuna kazi kubwa ya kujenga nchi yetu kuhakikisha mambo yanakwenda kwenye mstari unaotakiwa. Tuna kazi ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana kwa kusimamia vyema rasilimali zilizopo zinufaishe wananchi wote kupitia huduma za kijamii.


**Mungu ibariki Tanzania**





HAKIKA ILIKUWA FURAHA TELE KWA FREDDY MTAVANGU NA PENDO RAPHAEL, PALE WALIPOKUBALIANA KUWA MWILI MMOJA KWA KUFUNGA NDOA KATIKA KANISA LA ADVENTIST LILILOPO MBEZI BEACH, JIJINI DAR ES SALAAM HIVI KARIBUNI.





# MITINDO

Na Christina Mwakangale



# MITINDO YA NYWELE Inayowapagawisha wanaume

SUALA la mitindo linawagusa moja kwa moja wanaume ambao wanapenda kuwa na mwonekano mzuri na kujimiani.

Ukiacha mavazi na mapambo, mitindo ya nywele inaonyesha jinsi gani mtu alivyo mtanashati.

Wataalamu wa masuala ya mitindo wanasema nywele ni kiungo muhimu katika usafi ni alama muhimu katika kujionyesha na kujielezea mbele ya jamii.

Hata hivyo nywele zinatakiwa kuwekwa katika mitindo tofauti ambayo mtu husika anapenda ili kujiweka katika mtazamo mzuri.

**I. Kukata nywele**

Aina hii ya mtindo wa utunzaji wa nywele unafahamika na wengi, watu wanakata nywele saluni au kwa kinyozi anayetumia mkasi.

Ukataji wa nywele unamfanya mtu kuwa huru na inampunguzia gaharama ya kununua vipodozi kama akiwa na nywele ndefu.

Unashauriwa wakati wa kukata nywele hakikisha unampata kinyozi anayejua kazi yake kwani ni muhimu mitindo ya nywele ilingane na aina ya kichwa cha mhusika.

**2. Kunyoa 'Unga'**

Ni aina ya utunzaji wa nywele unaopendwa na watu maarufu kama baadhi ya viongozi wa nchi mbalimbali, wanasiasa, wafanyabiashara, wasanii na wana michezo.

Utunzaji wa nywele za aina hii rahisi sana na mara nyingi mhusika anahitaji kupaka mafuta ya kawaida ambayo hayana gharama.

Hata hivyo, endapo utachagua kunyoa unga unatakiwa kuwa na usafi wa hali ya juu, kwani kichwa kinaachwa kikiwa huru kiasi cha kuonyesha ngozi.

**3. Wave na Black**

Mtindo wa nywele wa kupaka dawa maalum ya kuweka mawimbi 'Wave' inahitaji gharama na muda zaidi wa kuziangalia.

Mara nyingi mtu akiweka wave na kuongeza rangi nyeusi 'Black' anahitaji kununua mafuta ya ziada kwa ajili ya kung'arisha na kuzuia nywele kukatika.

**ACHIA NYWELE**

Mtindo huu humfanya mtu kuwa na uasilia zaidi, anavutia machoni na kujiamini.

Nywele zinatakiwa kuwa ndefu ili kuzifanya zitawanyike vyema kama vile miale ya jua na hivyo kuongeza ladha ya mwonekano.

Hata hivyo, mtindo huu unahitaji umakini kwani nywele zinahitaji matunzo ya hali ya juu ikiwamo mafuta ya kulainisha, virutubisho na kuziosha kila wakati kuondoa uchafu.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# NGUVU YA YAI

## hung'arisha ngozi,huondoa madoa



YAI limekuwa na matumizi kama chakula kwa muda mrefu, lakini kuna matumizi mengine ambayo yana manufaa kwa binadamu.

Katika urembo yai linafanya kazi kikamilifu katika kurutubisha ngozi, nywele na pia kuondoa uchovu.

Kama unatamani kutumia yai ili kuboresha muonekano wa ngozi na nywele zako fuatilia maelezo yafuatayo.

Chukua yai, changanya na asali kijiko kimoja cha chai na mafuta ya olive.

Mchanganyiko huo ukiwa tayari paka usoni na shingoni, na subiri kwa dakika 10 hadi 15.

Hii itasaidia kama una mashimo usoni yatokanayo na chunusi kubana. Pia itasaidia kulainisha ngozi yako na kuwa nyororo.

Mchanganyiko huu utasaidia kukuondolea michubuko au alama za kuungua na jua na mafuta usoni.

Unaweza kutenganisha kiini cha yai na ule ute mweupe, kisha chukua ute weka kwenye kikombe au bakuli, baada ya hapo pigapiga ule ute hadi uwe na mapovu kisha chukua povu, linawe usoni au paka mwili mzima kisha acha ikauke.

Baada ya hapo osha na maji ya uvuguvugu, ukifanya hivyo mara kwa mara itakusaidia ngozi yako iwe angavu.

Kama umetoka kazini na unaonekana umechoka na unataka kutoka usiku, chukua ute wa yai na pakaa chini ya jicho na uache kwa dakika 10 hadi 15, kisha safisha. Njia hiyo inasaidia kuondoa muonekano wa uchovu katika macho yako.

Maski ya yai ina utajiri wa 'Acid' za Amino ambazo husaidia kupunguza na kuondoa miunguzo au muwasho mwilini kutokana na protini inayopatikana kwenye yai.

Kama unawashwa mwili mzima, chukua ute wa yai kidogo halafu nyunyiza katika maji utakayoyaoga sambamba na sabuni ya kuogea ndani ya siku chache utaona matokeo.

Kwa upande wa nywele wale ambao, nywele zao hazina afya au ukuaji wao ni hafifu wanaweza kupaka yai kichwani, hakikisha inagusa mizizi inayosaidia kuotesha nywele, kama nilivyoeleza awali protini iliyopo kwenye yai ndio chanzo cha kila kitu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia nyama ya kusaga



KUNA mapishi tofauti ya nyama ya kusaga, kabla ya kupika wengine wanaiosha wanachuja maji, kuna wanaochemsha, lakini mimi leo naipika tofauti.

Mahitaji

Nyama ya kusaga kilo moja, vitunguu maji viwili, vitunguu saumu viwili, tangawizi , nyanya nne, mafuta robo lita, chumvi kijiko kimoja cha chai, karoti mbili, pilipili hoho moja na ndimu moja.

Namna ya kuandaa

Menya vitunguu na ukate kwenye vipande vyembamba sana, menya na kwangua karoti iwe kama uji na pilipili hoho na kisha kata vipande vyembamba.

Menya nyanya na zikate kawaida, osha na kisha kwangua tangawizi na twanga vitunguu saumu. Weka sufuria jikoni, weka nyama na anza kukoroga ili kuzuia isigandie kwenye sufuria na kuungua, halafu weka kitunguu maji huku ukiendelea kukoroga kwa muda wa sekunde 10.

Weka kitunguu saumu na tangawizi na endelea kukoroga kwa muda wa sekunde tano zaidi, weka mafuta kidogo ili kufanya viungo viive.

Weka pilipili hoho, karoti na kamulia ndimu. Ongeza chumvi kidogo. Endelea kukoroga.

Weka nyanya, koroga na funika sufuria na mfuniko kwa muda kama dakika 10, funua angalia kama imeiva.

Mboga yako itakuwa tayari kwa kula na aina yoyote ya chakula utakachopendelea.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Kuwa mbunifu kupangilia nyumba ya nafasi ndogo

## Namna ya kuchagua viyoyozi ndani ya nyumba



ILI nyumba ipendeze inatakiwa kuwa na mashine za viyoyozi vya kisasa kwa ajili ya kupoza joto. Unatakiwa kuwa makini wakati unatafuta mashine hizo ili upate inayolingana na thamani ya pesa yako.

Zifuatazo ni baadhi ya dondoo unazotakiwa kuzifuata wakati unataka kufanya chaguo sahihi.

- Aina ya kiyoyozi;
- Nguvu yake
- Kiwango cha kelele na matumizi ya nishati.
- Uwezekano wa kupoza haraka
- Kazi ya kunyonya hewa
- Uwezo wa kuchuja hewa

Vigezo hivi vinapaswa kufuatwa wakati wa kuamua ni kiyoyozi gani cha kuchagua katika nyumba. Ni vyema kuzingatia maoni ya wataalamu baada ya kuona mazingira ya nyumba.

ASILIMIA kubwa ya wakazi wanaoishi mijini, wanakaa katika nyumba za kupanga. Kutokana na hali halisi ya familia za kiafrika, ni chache sana ambazo huwa na uwezo wa kumudu kupanga nyumba yote au kubwa ya kutosheleza familia nzima.

Kama ilivyo desturi kwa familia hizo za kiafrika, nyingi huwa zinajumuisha zile kama zinavyojulikana kwa lugha ya kigeni 'extended families', hivyo hivyo familia kuwa kubwa pasipo kulingana na kipato kilichopo cha kumudu kupanga nyumba kubwa.

Kwa hiyo ili umudu kuishi katika sehemu ndogo ya nyumba kulingana na uwezo uliopo na ukubwa wa familia, lazima ubunifu na akili nyingi vitumike katika kupangilia vitu ili nafasi katika nyumba hiyo itosheleze mahitaji.

Pia kuna haja ya kupunguza kuweka ndani ya nyumba baadhi ya vitu visivyo vya lazima.

Kwa upande wa uwekaji wa samani katika nyumba hiyo ndogo ni lazima uhakikishe zenye umbo dogo na ambazo zitakuwa na sehemu ya kuhifadhia vitu vingine au zenye matumizi zaidi ya moja.

Kwa mfano meza ya televisheni, unaweza kuweka ambayo inakuwa na matumizi ya kuwekea TV na pia kwa kuhifadhia vitu vingine hususani vitabu na vinginevyo.

Pia kutumia sehemu ya ukuta 'kudizaini' kwa ajili ya kuwekea vitu vingine ikiwamo vyombo hasa jikoni.

Ili ufanikishe kwa vitu vichache unavyokuwa umepanga kuweka kwenye nyumba hiyo ndogo ni vizuri kupima kwanza ukubwa wa eneo lako kabla ya kutengeneza samani zako.

Epuka kuweka vitu hovyo bila kufanya tathmini ya uhakika, na ikiwezekana orodhesha idadi ya vitu na vya aina gani vinavyotakiwa kuingia kwenye nyumba hiyo na ambavyo havichukui nafasi kubwa.





Tumia ubunifu katika sehemu za kona za nyumba yako kuweka fenicha zako, hususani meza na televisheni na uhakikishe nazo zinakuwa ni zile ambazo hazichukui nafasi kubwa.


Jambo kubwa la kuzingatia katika suala la kupangilia vitu katika nyumba yako ndogo ni ubunifu na kuepuka vitu ambavyo havina ulazima.

Usiweke kitu ilimradi umeona kwa jirani yako ameweka, isipokuwa kwa kuzingia umuhimu wake na nafasi uliyo nayo kwenye nyumba yako.

Pia katika siku za hivi karibuni kwa upande wa samani za ndani, zipo hata ambazo unaweza kuzikunja, na kama ukifanikiwa kupata za namna hiyo inakuwa bora zaidi katika kuhifadhi nafasi.

Kwa mantiki hiyo, unazitumia pale unapoona inahitajika tu, na unaweza kuamua kuzikunjua nyakati za mchana halafu usiku ukakunja.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
KWANI KAKA HUJAWAHI KUSIKIA 'GEMU IMEAHIRISHWA' KUTOKANA NA SABABU KAMA HII TUNAYOIONA AU SIO KAKA'ANGU?
SIO KWA BIA ULIZO-NINYWEA
BONDENI
ACHA KUNIPIGA SIASA, HAKUNA PESA ZA KULIPANA BAR.
UOGA TU. KULIPANA BAR KUNA FAIDA USIBISHE
DUME ZIMA UGOMVI WA USIKU UNAKUJA NAO MPAKA MCHANA! LETE HELA YA KULA
TAFUTA NENO LAINI
ABIRIA JADILINI YANAYOWAHUSU, HAYO YAKUPIGWA VYETI DABODABO MUYAACHE.
MMEZIDI KUHARIBU SHERIA MBUZI NYIE!
EBANAEE! UTASHUKA USHAANZA KUTUITA MBUZI TUKI-KUCHEKEA UTATUKANA!
USITUFUMBE MIDOMO WEWE ENDESHA GARI
SISI TUNGE-YAJUAJE?
HII NI OFISI LAZIMA SISI WENYEWE TUJADILIANE LAKINI SIO NA NYIE ABIRIA
CHAKULA ULICHO-NIAGIZA UNATAKA KUWEKA 'STOKU' NYUMBANI KWAKO AU KUNITIBIA?
'NI MWIKO' KUHOJI MAAGIZO YA MIZIMU HATA UKIAGIZWA FUSO USIHOJI.
UMESHINDWA KUTUMIA CHIPSI MAYAI KUTATUA MGOGORO WA NDOA MPAKA UNATUMIA 'MAGUMI KWA MKEO?'
MPAKA NIMEKUWA MEMBA KWA WAUZA CHIPSI, LAKINI BADO "HAKIELEWEKI!"
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKITAKA KUJUA UMUHIMU WA JIRANI KAISHI MSITUNI...

# Marekani yaionya China kuisaidia Russia

## ■Rais Ukraine aomba mazungumzo
## ■Madaraja yavunjwa kuilinda Kyiv

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amemuonya kiongozi mwenzake wa China Xi Jinping, kuhusu athari zitakazoikabili nchi yake endapo itatoa msaada wa vifaa kwa Russia katika uvamizi wake nchini Ukraine.

Biden ametoa onyo hilo wakati wa mazungumzo yake kwa njia ya video na Rais Xi, yaliyogusa mzozo wa Ukraine. Msemaji wa Ikulu ya Marekani White House Jen Psaki, alisema Rais Biden, alielezea jitihada za Marekani na washirika wake katika kushughulikia uvamizi wa Russia, ikiwemo kuiwekea vikwazo vikali.

Wizara ya Mambo ya Nje ya China, iliandika kwamba Rais Xi alimueleza Biden, juu ya kukomeshwa vita ya Ukraine haraka iwezekanavyo na kutoa wito kwa jumuiya ya kujihami NATO kufanya mazungumzo na Russia ili kushughulikia kiini cha mzozo wa Ukraine na kupunguza wasiwasi wa usalama wa mataifa hayo jirani.


Wakati huo huo, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ametoa wito wa kufanyika mazungumzo ya kina ya amani na Russia, akisema ndiyo nafasi pekee ya kupunguza uharibifu uliotokana na makosa ya uvamizi.

Zelensky alisema Ukraine ilikuwa ikitoa suluhisho kila wakati la amani na kutaka mazungumzo yenye maana juu ya usalama bila kuchelewa.

Kulingana na Zelensky vikosi vya Russia vinazuia kwa makusudi usambazaji wa misaada ya kiutu katika miji iliyoko chini ya mashambulizi.

Rais huyo alisema hadi sasa hakuna taarifa za watu wangapi wamefariki baada ya jumba la maonyesho kushambuliwa mjini Mariupol.

Wakati akitoa wito huo, vikosi vya Russia vimezidisha mashambulizi katika miji ya Ukraine ikiwa ni pamoja na mji mkuu, Kyiv na kituo cha ukarabati wa ndege nje kidogo ya mji wa Lviv, karibu na mpaka na Poland.



Baadhi ya wakazi wa Kyiv wakibeba silaha sambamba na wanajeshi wa Ukraine, katika harakati ya kuulinda mji huo usiangukie kwa vikosi vya Russia. **PICHA: AFP**

### RUSSIA YARUSHA KOMBORA LA HYPERSONIC

Msemaji wa wizara ya ulinzi ya Russia amesema kuwa Moscow imeharibu bohari ya chini ya ardhi magharibi mwa Ukraine kwa kutumia makombora ya hypersonic ambayo yanakwenda kwa kasi kuliko sauti.

Igor Konashenkov, alidai kuwa ghala hilo lilikuwa na makombora na risasi za anga za askari wa Ukraine.

Russia haijawahi kukubali kutumia makombora ya hypersonic katika mapigano hayo.

"Walipiga makombora makali ya balestiki ambayo yanaweza kuruka katika anga ya juu kwa zaidi ya mara tano ya kasi ya sauti," alisema.

Kwa mujibu wa jeshi la Russia, mfumo wa makombora wa "Kinzhal" uliotumika katika shambulio hilo una uwezo wa kulenga shabaha katika umbali wa zaidi ya kilomita 2,000 (maili 1,242) na unaweza kushinda mifumo yote ya ulinzi wa anga wa makombora.

### MKAKATI WA KUULINDA MJI WA KYIV

WAKATI Russia imethibitisha kutumia kombora la hypersonic dhidi ya ghala la silaha magharibi mwa Ukraine, bado majeshi yake yanapambana kuuweka mji mkuu wa Kyiv katika himaya yao.

Vita ya Russia na Ukraine inafikia siku ya 23, huku mashambulizi makali ya anga yakizidi kuteketeza miji mbalimbali ya nchi hiyo na hakuna dalili ya kumalizika katika kipindi kifupi kijacho.

Hata hivyo, majenerali wawili wa Ukraine wanaohusika na kuulinda mji wa Kiev wanaiambia BBC, kuwa vikosi vyao vinapambana kwa bidii ili kuwazuia wanajeshi wa Russia wasiingie katika mji huo.

Kiev inaathirika zaidi na vita hiyo, kutokana na kukabiliwa na silaha za nguvu zenye uharibifu Russia.

Lakini katikati ya Kiev na vitongoji vyake vingi bado havijaguswa na silaha za Russia. Miji mingine ya Ukraine inashambuliwa kwa mabomu na kumekuwa na majeruhi wengi.

Majenerali hao wanaohusika na ulinzi wa Kiev walisema Ukraine inapambana kwa nguvu, lakini walikiri kwamba mji mkuu huo uko katika hatari ya kushambuliwa na makombora.

Hata hivyo, walisema itakuwa vigumu kwa Warussia kuuchukua mji huo kutokana na eneo la juu la mji huo kuwa la aina yake.

Jenerali Andriy Kryschenko, alisema mji huo mkubwa umegawanywa na mto mkubwa unaoitwa Dnieper. Pia kuna mito midogo inayoingiza maji yake humo ambayo imetenganisha maeneo ya mji huo kipekee.

"Ni vigumu kuulinda kote, ikizingatiwa kuwa ni mji mkubwa sana, lakini kwa upande mwingine, ni faida kwetu. Mito na madaraja yako kwenye milango ya mji. Wanajeshi wetu wanaweka ulinzi ." Alisema Jenerali huyo

Aliongeza "Karibu na mji kuna mito mingi midogo ambayo hutiririka kuingia mto Dnieper na kuna maeneo tepetepe ambayo inamaanisha kuwa eneo hilo halifai kwa harakati kubwa za kijeshi."

Jenerali Kryschenko, ambaye pia ni naibu meya, amekuwa akivaa mavazi ya kawaida ya kijeshi kama ambayo rais wake Volodymyr Zelensky amekuwa akivaa anapozungumza na watu wake, kuwavutia washirika wake na kuwakasirisha maadui zake.

Faida nyingine, Kiev ni mji wa viwanda, ambapo viwanda na karakana hizo zimekuwa sehemu muhimu ya kutengeneza ngome, matofali ya saruji, mifuko ya mchanga na vikwazo mbalimbali vya kupambana na vifaru.

Jenerali Andriy Kryschenko, alieleza eneo linalozunguka Kyiv linawafanya wanajeshi wengi wanaotaka kuingia katika mji huo kupata shida.

Viongozi hao wa kijeshi walisema kutokana na jiografia hiyo, wamefanikiwa kuzuia mashambulizi makubwa mawili: moja kutoka mashariki na moja kutoka kaskazini magharibi, ukiwemo msururu mkubwa wa magari ya kivita ya Russia ambayo yamekwama kilomita 64.

Kaskazini magharibi mwa nchi hiyo bado kunalengwa zaidi na Russia, ambako ni upande wa pili wa Mto Irpin, karibu kilomita 20 kutoka katikati ya Kiev.

Ukraine imepeleka vikosi vyake vilivyojipanga vizuri na vyenye silaha nzuri, ambavyo vilibomoa madaraja ya kimkakati.

Maelfu ya watu waliokimbia makazi yao kutoka mji wa Irpin wamekuwa wakivuka mto huo kwa kupita juu ya mabaki ya daraja lililovunjwa, wakiwa na mbwa na paka wanaowamiliki.

Lakini Jenerali Knyazev alisema: "Hii ni ardhi ya ajabu sana, na hawawezi kupitia. Kama kusingekuwa na wanajeshi wetu katika eneo hilo la mto, wangeshambulia daraja kirahisi. Lakini tuko pale na tunataka kuwaangamiza."

Mafanikio ya kijeshi ya Ukraine yamewashangaza washirika na maadui zake. Rais na makamanda wake wanafurahishwa zaidi na utendaji wa jeshi lao na maelfu ya watu wa kujitolea.

Hata hivyo Warussia bado hawajaweka nguvu zao kamili katika mji huo mkuu.

MAKALA

# MATUMIZI MABAYA MITANDAO YA KIJAMII YATAKUHUKUMU



Na Magabilo Masambu - 0689157789

NI kweli kwamba mitandao ya kijamii kama Facebook, Twitter, Youtube, WhatsAap, na Instagram, imerahisisha sana mawasiliano yetu. Leo kwa kutumia mitandao hiyo tunaweza kuwasiliana na yeyote duniani, tunaweza kutuma ujumbe mfupi wa maneno (sms), kutuma picha ama video au kupiga simu na kufanya mazungumzo.

Nje ya mawasiliano, wako wanaoitumia mitandao hiyo kibiashara ama kuuza bidhaa zao moja kwa moja, kutangaza au kufanya mawasiliano na wafanyabiashara wengine duniani. Lakini pia inatumika kuonyesha uwezo na vipawa vyetu. Mfano, kama una kipawa cha uimbaji, uigizaji, uandishi, siasa na kila aina ya sanaa, unaweza kuwaonyesha watu uwezo wako kirahisi.

Kinachosikitisha ni kwamba pamoja na faida zote hizo, wako wanaoamua kwa hiari yao kutumia mitandao ya kijamii kinyume cha maadili yetu kama Watanzania. Ama kwa kujua au kwa kutojua madhara yake ya leo na kesho yao, wanatuma picha au video za utupu mitandaoni bila kujali kwamba wana ndugu, jamaa na marafiki watakaozitazama.

Jambo ambalo hatulijui ni kwamba maisha ya mwanadamu ni fumbo kubwa kwa sababu tunajua tulikotoka lakini hakuna yeyote miongoni mwetu anayejua tunakokwenda. Hakuna anayeijua kesho yake. Tunaweza kudhani kwamba tulipo tumefika kumbe Mungu anakuwa na mipango mingine na sisi. Wako watu ambao wanajiona waimbaji, waigizaji, wachekeshaji, waandishi na kadhalika na wamejiridhisha kwamba maisha yao yatakuwa hayo.

Mipango ya Mungu ni mikubwa huwa anamwinua yeyote. Unaweza kuwa mchekeshaji leo kama Steve Nyerere kesho ukawa Rais wa nchi kama alivyo Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky. Unaweza kuwa mchezaji mzuri sana wa mpira leo kama Samata, kesho ukawa Rais kama George Weah wa Liberia. Unaweza kuwa mwanamitindo leo kama Hamisa Mobeto kesho ukawa mkuu wa wilaya kama Jokate Mwegelo. Siwezi kutaja wote lakini itoshe kusema kwamba yeyote anaweza kuwa chochote.

Ninachotaka kusema ni kwamba nafasi tulizo nazo leo tusione hatuwezi kuwa wengine kesho maana yake matukio tunayoyafanya tukiwa na nafasi hizi leo, tuyafanye tukiwa waangalifu kwamba kesho na keshokutwa tukiwa watu mashuhuri kwenye jamii mambo yetu ya leo yasitufanye tukahukumiwa kesho. Ni mjinga tu atakayehukumiwa kesho utetezi uwe kwamba nilifanya hayo kwa sababu nilikuwa msanii au ilinilazimu kufanya hayo kwa wakati huo, lazima tutambue kwamba mitandao ya kijamii inahifadhi taarifa zetu milele.

Leo unapiga picha au video za utupu unazituma mtandaoni, kesho unakuwa Rais au kiongozi mashuhuri waungwana wanakukumbusha kwamba kuna kapicha kako hapa unakakumbuka? Unaanza kutumia vyombo vya usalama kuwaumiza wanaokukumbusha kwa mambo uliyoyafanya mwenyewe ukiwa na akili timamu. Nani atalaumiwa katika hilo kama si mwenyewe utajilaumu?

Hivi karibuni kumekuwapo na matukio machafu zaidi hasa yakiwahusu watoto wa kike. Baadhi wanatoa utetezi kwamba picha hizo zinavujishwa na watu wao wa karibu wakiwa na malengo wanayoyajua wao lakini kwa nini urekodi picha za namna hiyo na kumtumia mtu mwingine? Unadhani kufanya hivyo atakupenda sana?

Jambo usilolijua ni kwamba thamani ya mwili wako ni kubwa kuliko kitu chochote, kwa sababu matukio ya namna hiyo yanaweza kugharimu maisha yako, baadhi tumesikia wakijiuwa baada ya picha zao kuvuja.

Nakubali kwamba kwa sababu ya ukuaji wa teknolojia, inawezekana ukarekodiwa bila kuwa na taarifa lakini uzoefu unaonyesha walio wengi wamekuwa wakirekodi na kupiga picha wenyewe au kuwaamini watu wao wa karibu na kwamba watazitunza. Lakini inapotokea kutokuelewana wanaona silaha ya kukumaliza ni kuachia picha na video zako. Ni muhimu sana kujilinda kabla ya kulindwa na wengine, linda utu wako lakini zaidi heshima yako ya leo na ya kesho.

Wako wanaotumia picha zao kuongeza watazamaji kwenye mitandao yao ya kijamii na inawezekana inawapatia fedha kwa maoni yangu bado una uwezo wa kuongeza watazamaji kwa kulinda maadili, utamaduni na utu wako kwa sababu si watazamaji wote wanafurahia kuona picha za utupu. Fedha zinazopatikana kwa njia hiyo hazitakuwa tofauti na za ukahaba au uuzaji wa bangi.

Jambo ambalo wengi pia hawajalifahamu ni kwamba leo hii watu wengi wanakosa kazi duniani kwa sababu tu wamekuwa watumiaji wabaya wa mitandao ya kijamii. Unakwenda kuomba kazi kwenye kampuni fulani una vigezo vyote vya kielimu, lakini wanaotaka kukupatia kazi wanaona wajiridhishe kwa kulitafuta jina lako kwenye mitandao, wanakuta mambo ya ovyo. Matokeo yake wanakunyima maana wanaona wakikupatia kazi, unaweza kuharibu 'brand' ya kampuni yao.

Ushauri wangu kwa watumiaji wenzangu wa mitandao ya kijamii, ni muhimu matumizi yetu ya leo yalinde heshima yetu ya kesho. Tunaweza kuwa na watoto wadogo leo kesho watakuwa watu wazima. Tutawapa taabu sana watakapokuwa na wenzao au wenyewe kuzitazama picha na video zetu.

Ishi leo kwa matarajio ya kuwapo kesho, kazi yako leo isiue matumaini ya kuwa mtu mwingine kesho kwani lolote linawezekana. Ni jambo la muda tu.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Marijani Rajabu alipokacha ukipa Simba na kuwa mwanamuziki



Na Adam Fungamwango

MACHI 23, mwaka huu, Tanzania iliadhimisha miaka 27 ya kifo cha mwanamuziki maarufu, aliyelitangaza jina la nchi nje ya mipaka, Marijani Rajabu, aliyekuwa akijulikana kama Jabali la Muziki.

Alifariki dunia nyumbani kwake Kariakoo, mtaa wa Somali, karibu kabisa na maeneo ya Gerezani, na kuzikwa kesho yake kwenye makaburi ya Kisutu, Dar es Salaam.

Hadi leo, Marijani anabaki kuwa mmoja wa wanamuziki wachache nchini ambao bado wameendelea kuwa maarufu kizazi hadi kizazi hata baada ya kufariki dunia. Ni mwanamuziki aliyeimba nyimbo za maudhui yote zikiwamo za siasa, mapenzi, matukio, ukombozi barani Afrika na matatizo ya kijamii.

Alitunga na kuimba zaidi ya nyimbo 300 hadi kufariki dunia kwake. Baadhi ya nyimbo ambazo ni maarufu zaidi hadi leo hii na zingine zimerudiwa na wasanii wa kizazi kipya ni 'Zuena', 'Mwanameka', 'Siwema', 'Dunia Uwanja wa Fujo', 'Baruti', 'Masudi', 'Georgina', 'Ndoa ya Mateso', 'Pesa', 'Pombe si Chai', 'Pendo", 'Rufani ya Kifo', 'Ukewenza' na 'Uzuri wa Asili'. Hizo ni kwa uchache kwani ukiziorodhesha nyimbo zake hapa, unaweza kujaza ukurasa mzima.

Kutokana na kazi zake nyingi na umaarufu wa mwanamuziki huyo, unaweza kudhani kuwa alifariki dunia akiwa na umri mkubwa sana. La hasha. Alifariki dunia akiwa na miaka 40 tu. Alizaliwa Machi 3, 1955 na kufariki Machi 23, 1995 na kuacha vilio, simanzi na huzuni kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini.

Marijani alianza muziki akiwa bado mdogo akiwa anasoma, kitu ambacho kilimletea matatizo yeye mwenyewe na bendi ambazo amepigiwa mwanzo kama tutakavyoona baadaye, lakini pia alikuwa na kipaji kingine cha kucheza mpira.

Alikuwa golikipa mahiri wa Shule ya Sekondari ya Tambaza alipokuwa akisoma, huku pia akipiga muziki, lakini mitaani alikuwa akidakia timu mbalimbali, huku timu yake kubwa ikiwa Kahe FC. Umahiri wake ulimfanya aanze kuwindwa na klabu ya Simba kwenda kuidakia, huku mwenyewe akiwa ni mpenzi wa klabu hiyo na alikubali.

Kwa mujibu wake mwenyewe wakati wa uhai wake akihojiwa, alisema hakwenda Simba kwa sababu tayari alishachagua muziki kama kazi yake halisi badala ya mpira, kwani awali alikuwa hajui aende wapi kati ya muziki na mpira, huku vitu vyote viwili akivifanya kwa uwezo sawa.

Marijani alitoka nje ya Tanzania kwa mara ya kwanza ambapo alikwenda Nairobi na kurekodi nyimbo zilizotoka katika lebo ya Phillips. Hili jambo la mwanafunzi kusafiri na bendi likaleta shida na kwa vile (STC) ilikuwa mali ya umma, akatimuliwa mwaka 1972, lakini alijiunga na Safari Trippers ya David Mussa ambayo kwa wakati huo ilikuwa inapiga zaidi nyimbo za hoteli na za kukopi na mwimbaji wao kiongozi wakati huo alikuwa Ali Rajabu.

Hapa ndipo ubora wake ulifunguka hasa na kuinyanyua Trippers, kwani walitoa vibao vilivyopendwa mfululizo na kuzunguka nchi nzima. Baadhi ya vibao hivyo ni kama Rosa Nenda Shule, Georgina, Mkuki Moyoni ambavyo viliuza zaidi ya nakala 10,000 za santuri, hivyo kuwezesha bendi kuwa na vyombo vyake vizuri.

Mwaka 1976, Marijani na baadhi ya wanamuziki wa Safari Trippers waliamua kuihama bendi na kwenda kuasisi Dar es salaam International chini ya umiliki wa Mzee Zakaria Ndabemeye. Baadhi ya wanamuziki hao ni Abel Baltazar kutoka Msondo, Kassim Mponda kutoka Trippers, Abdallah Gama, Joseph Mulenga, Haruna Lwali na George Kessy Omojo waliokuwa wanapiga muziki Margot pale, Said Mohamed kutoka Polisi Jazz, Cosmas Chidumule kutoka Urafiki, Belesa Kakere kutoka Biashara Jazz, Joseph Bernard kutoka Trippers, Ali Rajabu kutoka Trippers, na King Michael Enock kutoka Dar es Salaam Jazz.

Akiwa Dar International alishiriki kutunga nyimbo mbili, Betty na Sikitiko. Hata hivyo kama waswahili wanavyosema mafahali wawili hawakai zizi moja, ndivyo ilivyotokea kati yake na Abel Balthazal kiasi cha hatimaye Marijani kufukuzwa ndani ya bendi kutokana na ubishi kuhusu wimbo aliotunga. Kuna maelezo kuwa wimbo ulionekana unafanana na wimbo fulani toka Congo na hivyo Marijani akatakiwa aubadilishe na ndipo ugomvi ukaanza.

Hata hivyo, mwishoni mwa mwaka 1978, Marijani alirejeshwa tena kundini kutokana na rundo la wanamuziki wa Dar International kuihama bendi kwa kishindo na kwenda kuanzisha bendi mpya kabisa ya Orchestra Mlimani Park. Aliporejeshwa Marijani alikuja na wanamuziki wengi wapya wakati huo kama Christopher Kasongo, Mohamed Tungwa, Mafumu Bilal, Hamis Milambo, Athuman Momba na Mzee Alex Kanyimbo na kuja na mtindo wa Super Bomboka.

Katika kudhihirisha hasira zake kwa Barthazal, Marijani alimtungia wimbo wa 'Kidudu Mtu' ambao Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD) waliukataa kuurekodi, jambo lililokuwa kawaida enzi hizo kwa redio kukataa wimbo. Miongoni mwa wanamuziki waliohamia ni Fresh Jumbe, Mohamed Mwinyikondo, Juma Choma na Tino Masinge.

Hata hivyo safari ya Dar International ilikoma mwaka 1987 kutokana na sababu za kawaida za kufa kwa bendi, kubwa ikiwa uchakavu wa vyombo. Hata hivyo, Marijani aliendelea kufanya muziki na kwa kipindi kifupi amewahi kupigia Kurugenzi Jazz ya Arusha, Juju Masai pia ya Arusha na Mwenge Jazz ambayo alirekodi nayo wimbo mmoja wa Ukimwi na hata kupitia bendi ya Watafiti.

Aidha mwaka 1991 aliwahi kurekodi 'zong zing' na marehemu Eddy Sheggy.

Bendi yake ya mwisho ilikuwa Africulture au Mahepe Ngoma ya Wajanja, iliyokuwa mali ya Rogers Malila, alikokuwa na wanamuziki kadhaa kama Hassan Kunyata ma Mgosi na wengine.

Pamoja na kwamba ni takriban miongo mitatu tangu alipofariki dunia, bado Marijani ataendelea kukumbukwa na wapenda muziki kote nchini na Afrika kwa ujumla kwa nyimbo zake tamu na zenye mafundisho.

# HADITHI

# Ajenda ya Siri-22

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

SASA ukafika wakati wa upande wa utetezi kutoa ushahidi wao kuonyesha vielelezo vyao ambavyo vinaweza kuonyesha kama Tina huenda hakuwa peke yake kwenye kesi hiyo, alishawishiwa kwa kujua au bila kujua na nia kubwa ni kumpunguzia angalau adhabu inayomkabili ya kunyongwa hadi kufa.

'Nondo' zilizoletwa mahakamani hapo zilikusanywa na mpelelezi Eddy Kamal na kuwasilishwa kwa Wakili Florence Tinga ambaye naye alizipeleka mahakamani hapo kama ushahidi upande wa utetezi.

Ushahidi ulianza kwa kuonyesha kuwa Tina aliondoka nyumbani hapo saa nne asubuhi kwenda kununua dawa. Alikwenda kununua dawa ambazo ndizo zilizowekwa kwenye chakula alichokula marehemu Chilambo.

Ni kweli kama upande wa mashtaka ulivyotoa ushahidi kuwa mshtakiwa Tina alikwenda kwenye duka la dawa 'Ni Sisi Pharmacy' lililoko huko huko maeneo ya Tegeta na alinunua aina mbili za dawa ambazo ukizichanganya kwa pamoja zinageuka kuwa sumu kwa binadamu au kiumbe chochote chenye uhai.

Ushahidi wa awali wa Mwahija Chota ulithibitisha hilo. Ushahidi upande wa utetezi ukapigilia msumari kuwa yote hayo yalikuwa sawa.

Upande wa utetezi, ukaendelea kumwaga 'nondo' zake kuwa baada ya kununua dawa hizo, Tina alikuwa anarejea nyumbani akiwa na dawa hizo, njiani akakutana na Abdallah Mtola. Kijana huyo alikuwa ndani ya gari. Alisimama na kuongea kwa dakika moja na Tina. Mshtakiwa alimkabidhi kifuko cha dawa hizo. Kwa hiyo Tina alirudi nyumbani akiwa hana dawa.

Kwa bahati mbaya sana, dawa ambazo alizinunua ndizo hizo hizo zilizokuja kumuua bosi wake Chilambo.

Kwa sababu yeye ndiye aliyezinunua kwenye duka la dawa na hizo ndizo zilizomuua Chilambo, ndio ushahidi uliotumika kumhukumu Tina. Mahakama haikuangalia au kujidhihirisha kuwa ni kweli alizifikisha nyumbani.




> **"Nakuomba ikipita ipige picha, ambayo namba zake zinaonekana na dereva pia kama sura yake inaweza kuonekana vizuri. Kama haikuwezekana piga gari tu, sehemu ambayo namba zinaonekana vizuri, halafu nitumie kwenye namba hii." Alimpa namba ya simu ambayo hutumia kwa masuala ya kijamii na si ya kikazi.**

Ushahidi wa watu wawili na vielelezo vyake vinathibitisha dawa hizo hakufika nazo nyumbani.

Kauli ya Mzee Mwayangu mwenye umri wa miaka 70 anayeishi Boko na kufanya biashara zake karibu na duka la dawa alilokwenda Tina, kama alivyohojiwa na mpelelezi Eddy Kamal wakati wa upelelezi wake ulithibitisha hivyo.

"Nilisalimiana naye, akaenda kwenye duka la dawa, aliporudi nilimuuliza unaumwa? Akanijibu hapana, dawa hizi siyo zangu. Za nani? Hakunijibu, alionekana kuwa na haraka."

"Wala hakusema nani anaumwa au ametumwa na nani?"

"Ila alipokuwa anaondoka, mbele kule nilimwona amesimama kwenye mlango wa gari, halafu likaondoka na yeye akawa anaendelea na safari zake, nikaona yule tayari ameshakuwa msichana mkubwa sasa, inawezekana amesimamishwa na mwanamume mwenye gari wanaongea, si unajua tena vijana."

Ingawa hakuwa na uhakika kwa asilimia mia moja kama Tina alimpa dereva wa gari hilo dawa, ushahidi wa kimazingira unaonyesha kuwa mshtakiwa alisimama njiani na mtu mmoja ambaye ni mwanamume. Upande wa utetezi umemtambua kijana huyo ni Abdallah Mtola.

Ushahidi mwingine ulioletwa mahakamani hapo ni wa kijana anayeuza na kukodisha CD anayeishi maeneo jirani ya hapo, aitwaye Nanje. Wakati Eddy akifanya upelelezi wake alipitia kwake na kumhoji maswali kadhaa yaliyomfanya kupata ushahidi ambao umewasilishwa mahakamani hapo.

"Wewe unadhani ni kweli alimuua bosi wake? Siamini. Sikiliza nikwambie. Mimi nilimuona siku ile alipotoka duka la dawa. Si wanasema alimuua kwa dawa za dukani zilizochanganywa na kuwa sumu, siku ile nilimuona, alitoka kununua kwenye duka moja lipo mbele pale, alipofika hapo nje, akakutana na gari moja lilikuwa limesimama, nikaona kabisa anampa kile cheti na dawa, halafu yeye akarudi nyumbani, jamaa aliyekuwa kwenye gari akaondoka kuelekea sehemu nyingine."

Yalikuwa ni mazungumzo ya kijana huyo Nanje na Eddy siku alipokwenda kuuliza ili kukusanya ushahidi. Na ndiyo siku ambayo Eddy alimpa kazi Nanje kulipiga picha gari la huyo jamaa aliyepokea dawa hizo kutoka kwa Tina.

"Unamfahamu mtu huyo?"

"Hapana, ila mara moja moja huwa anapita na gari lake. Nina wasiwasi sana na mtu huyo."

"Ni gari ya aina gani?"

"Toyota Alphard ya rangi nyeupe."

Eddy akitoa noti tano za shilingi elfu kumi na kumkabidhi kijana yule.

"Usimwambie mtu yeyote hii habari. Ila wewe si una simu ya tachi?"

"Ndiyo"

"Nakuomba ikipita ipige picha, ambayo namba zake zinaonekana na dereva pia kama sura yake inaweza kuonekana vizuri. Kama haikuwezekana piga gari tu, sehemu ambayo namba zinaonekana vizuri, halafu nitumie kwenye namba hii." Alimpa namba ya simu ambayo hutumia kwa masuala ya kijamii na si ya kikazi.

"Poa braza, nimekusikia, nitaifanya kazi hii, yaani umenipiga tafu sana na hii pesa." Yalikuwa maongezi wakati Eddy akikusanya ushahidi wake na ni moja ya picha ambayo iliwasilishwa kama kielelezo mahakamani hapo.

Ina maana Nanje alifanya kazi aliyotumwa akalipiga picha, akamtumia kwenye simu yake, akimjulisha kuwa huyo ndiye mtu ambaye alisimama na Tina siku hiyo na ndiye aliyekabidhiwa dawa hizo. Ushahidi wa Nanje ni kwamba gari lilikuwa hilo hilo na mtu ni yule yule.

Mpigaji picha alikuwa mahiri kwani hata sura ya dereva ilionekana vizuri tu pamoja na namba zake za usajili, Eddy alikuja kuliona kwa macho yake kwenye 'pub' ya Fabrice huko Tegeta, siku aliyoahidiana kukutana na Mwahija.

Alipoliona alilifananisha na gari ambalo lipo kwenye picha aliyopewa na Nanje. Na kweli alipoangalia hata namba zake zilifanana na lile gari lenye rangi nyeupe aina ya Toyota Alphard ambalo picha ilitumwa kwake.

Itakumbukwa aliingiza mkono mfukoni na kutoa simu yake ya mkononi. Akatafuta picha moja akaiangalia. Ilikuwa picha ya gari lile. Na namba zilikuwa zile zile. Aliisaka picha nyingine aliyokuwa na wasiwasi nayo. Nayo ilikuwa picha ya gari lile lile.

Aliteremka dereva kijana ambaye aliyeonekana na umri kati ya miaka 26 na 30 hivi. Alivaa suruali aina ya Jeans na fulana ya rangi ya bluu. Alishuka ndani ya gari hiyo peke yake. Bila hili wala lile aliingia kwenye pub hiyo.

Akaipiga picha gari hiyo, akawa na picha tatu ya gari lile lile zilizopigwa sehemu tatu tofauti. Ndilo lililopigwa picha na Nanje na yeye mwenyewe aliwahi kulipiga picha kabla.

ITAENDELEA JUMAPILI

## HABARI BURUDANI



# FELIS MUBIBYA MWAFRIKA ANAYETAMBA MUZIKI WA INJILI

KATIKA chati za muziki nchini wimbo wa 'Kata Dance' ulioimbwa na Felis Mubibya, unaonyesha kufanya vizuri kila kukicha.

Mwimbaji huyo mwenye asili ya Congo DRC, ametafutwa na gazeti hili na kufanyiwa mahojiano maalumu kwa simu, ambapo ameeleza mengi kuhusu muziki na maisha yake kwa ujumla.

**SWALI: Ndani ya wimbo 'Kata Dance' kuna ujumbe gani ulitaka mashabiki waupate?**

**Felis:** 'Kata Dance' ni sauti kutoka kwenye moyo wa shukrani, moyo unao mtukuza Mungu kwa ajili ya uungu wake na sio tu kwa ajili ya kile alicho kifanya.

**SWALI: Kwanini umeamua kutangaza zaidi muziki wako ndani ya Afrika na sio huko Marekani unapoishi?**

**Felis:** Katika ahadi aliyoiacha Yesu kwa wanafunzi kwenye ile Matendo ya Mitume 1:8, " Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika Uyahudi wote na Samaria na hata mwisho wa nchi "

Ni kweli kwamba tumeitwa kupeleka neno la Mungu kwa mataifa yote lakini kuna umuhimu wakuanzia nyumbani.

Hata hivyo, mwaka juzi nilifanya albamu ya Kiingereza inayoitwa 'Story of Courage' maalumu kwa ajili ya Marekani na Ulaya kwa hiyo ni vyema basi nyumbani tucheze.

**SWALI: Kwa shabiki mpya ambaye hajapata bahati ya kukufahamu wewe ni nani?**

**Felis:** Felis Mubibya au nilivyo zoeleka huko Tanzania, Felis Mwambalo Mubibya ni mwimbaji wa nyimbo za injili.

Baada ya kufanya muziki nchini Congo nilikozaliwa nikaenda kufanya huduma Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na kisha Tanzania.

Albamu yangu ya kwanza niliitoa mwaka 2006 inayoitwa 'Yuko Njiani', 2008 nilitoa nyingine 'Yesu ni Mungu' chini ya lebo ya Family Studios na 2011 niliachia 'Jipe Moyo' ambayo ilifanya vizuri.

Baada ya kazi hiyo niliamua kurudi chuoni kumalizia shahada yangu ya Applied Art in Modern Music, nikijikita kwenye theolojia.

Sasa nina miliki studio inayoitwa Shabach Records ambayo ipo hapa Marekani na nimezalisha nyimbo nyingi.

Nimeoa na nina watoto watatu na wote ninaishi nao Chicago Marekani.

**SWALI: Je unapata ushirikiano wa kutosha kutoka kwa waimbaji wa Injili wa Afrika?**

**Felis**: Ndio. Nina uhusiano mzuri na wengi, haswa wale tuliofahamiana nao nikiwa bado Tanzania na hata wale tulio kutana baadae.

**SWALI: Mashabiki wanaweza kutumia njia gani kupata muziki wako? Na baada ya Kata Dance mipango yako ni ipi?**

**Felis:** Muziki wangu unapatikana kwenye digital platforms za Apple Music, iTunes, Spotify, Deezer, Amazon, Google Play na zingine nyingi.

# *Wasanii watakiwa kuzalisha kazi bora*

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imewataka wasanii kuzalisha kazi bora na kuzisambaza kwenye vituo vya redio na televisheni ili kunufaika na mapato yatokanayo na mirabaha.

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Mohamed Mchengerwa (pichani), amesema serikali kupitia Taasisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA), baada ya miaka minne kupita imefanyia kazi suala la mirabaha ya wasanii na kuongeza kipato kutokana na makusanyo.

Amesema kuanzia Julai mosi hadi Desemba mwaka 2021 walikusanya milioni 312.29 na kugawanywa kati ya kazi za sanaa 5924 zilizokidhi vigezo vya kupata mirabaha na wasanii 1123 walinufaika.

"Ni lengo la serikali kuendelea kugawa mirabaha hii kila baada ya miezi sita, niendelee kuwatia moyo wasanii kwamba lengo la serikali na maelekezo ya Rais Samia tutaendelea kufanya maboresho," anasema na kuongeza.

Pia amewataka baadhi ya wasanii ambao hawajapata mirabaha yao kwenda Cosota kwani idadi kubwa hawajaenda kuchukua haki yao.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADRID YAKATA TAMAA
MATUMAINI ya Real Madrid ya kuipiku Manchester City katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21 kutoka Borussia Dortmund yanazidi kufifia. ***(Goal)***

### SILVA KUREJEA BENFICA
KIUNGO wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 27, anafikiria kurejea katika klabu ya nyumbani ya Benfica katika miaka miwili ijayo. ***(Mail)***

### TUCHEL AIKANA UNITED
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel ametupilia mbali tetesi zinazomhusisha kutaka kuhamia Manchester United, akisema klabu yake ya Stamford Bridge "ina kila kitu kinachotakiwa kunifanya niwe na furaha." ***(Metro)***

### RODRI, CITY KIMEELEWEKA
KLABU ya Manchester City inatarajia kumwongezea mkataba kiungo wake wa Hispania, Rodri mwenye umri wa miaka 25 ambaye mkataba wake wa sasa unakwenda mpaka mwaka 2025. ***(Telegraph)***

### TIELEMANS AJIPANGA UPYA
KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 24 ambaye ana mkataba na Leicester City unaomalizika mwaka 2023, amesema mazungumzo yanaendelea kuhusu mustakabali wake. ***(Metro)***

### MESSI KURUDI BARCA
MLINZI, Dani Alves mwenye umri wa miaka 38, amesema mchezaji mwenzake wa Barcelona, Lionel Messi hafurahii maisha pale Paris St-Germain na anatumaini mshambuliaji huyo raia wa Argentina mwenye miaka 34 anaweza kurudi Nou Camp. ***(Mirror)***

### UNITED, MILAN VITANI
KLABU za Manchester United na Inter Milan zinamfuatilia mlinzi wa Fiorentina na Timu ya Taifa ya Serbia, Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Italia)***

### TCHOUAMENI AITAMANI EPL
REAL Madrid inavutiwa na kiungo wa Monaco, Aurelien Tchouameni lakini nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa anafikiria kuelekea katika Ligi Kuu England, huku klabu za Liverpool, Manchester City na Manchester United zikionyesha kuvutiwa na kinda huyo mwenye umri wa miaka miaka 22. ***(Marca)***

### DE GEA NJE HISPANIA
GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 31, ametemwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Hispania kitakachocheza mechi za kirafiki dhidi ya Albania na Iceland kwa sababu haendani na mfumo wa uchezaji wa timu hiyo. ***(Manchester Evening News)***

### SAVIO KUTUA CITY
MANCHESTER City imekubaliana na mpango wa pauni milioni 5.4 kumsajili mshambuliaji wa Atletico Mineiro, Savio mwenye umri wa miaka 17, ambaye anachezea timu za vijana za Brazil. ***(Goal)***

### BLAS NYOTA IMENG'AA
WEST Ham imeungana na Newcastle United kumfuatilia kiungo Mfaransa, Ludovic Blas mwenye umri wa miaka 24 ambaye anachezea Nantes. ***(Football Transfers)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VALVERDE AFURAHIA KIWANGO CHA BARCA

●●● Asema kimerejesha ari kuelekea mechi ya El Clasico itakayochezwa leo...

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Fede Valverde amefurahishwa na kile alichokiona kutoka Barcelona chini ya kocha, Xavi Hernandez.

Barca wameimarika sana chini ya Xavi, wakisaidiwa na wachezaji wapya kama Pierre-Emerick Aubameyang, Ferran Torres na Adama Traore, ambao walinunuliwa katika dirisha la majira ya baridi la Januari.

Mabadiliko chini ya Xavi yalianza taratibu baada ya kocha huyo kuingia klabuni hapo.

**Barca wameshinda mechi sita kati ya saba zilizopita, na sasa wako katika nafasi ya tatu kabla ya mechi ya El Clasico dhidi ya Real Madrid itakayochezwa leo.**

Pia walijihakikishia tiketi ya robo fainali ya Ligi ya Europa siku ya Alhamisi, wakiwashinda Galatasaray ugenini kwenye mechi yao ya pili.

Akizungumzia Barcelona, Valverde amesema; "Wanacheza vizuri sana. Wamekuwa na mabadiliko makubwa sana.

"Wanacheza vizuri sana na inaonyesha wanataka kwenda kutafuta pointi kwenye mchezo.

"Kwetu sisi, tuna mchezo wetu, tutaenda kutafuta kitu kwanza na tuna silaha zetu."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
BARCELONA
1 | 2.20
X | 3.49
2 | 3.15

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LOPETEGUI AKARIBIA KUTUA RASMI MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

MATUMAINI ya Manchester United kupata medali msimu huu yamepotea rasmi na sasa mwelekeo unaelekea katika msimu wa 2022-23.

Mashetani Wekundu wamesalia kuangazia vita vyao vya hatua ya nne bora kwenye Ligi Kuu England baada ya kuondolewa na Atletico Madrid katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hilo hakika limemaliza matumaini ya Ralf Rangnick ya kutwaa wadhifa wa ukocha wa muda wote, ingawa bado haijafahamika ni nani atakuwa kwenye kiti moto cha Old Trafford msimu ujao.

Makocha kama Mauricio Pochettino, Erikten Hag na Thomas Tuchel wametajwa kuwania kuchukua nafasi ya Rangnick, lakini jina lingine sasa linaweza kuwa kwenye sura hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la Hispania la Fichajes, kocha Sevilla, Julen Lopetegui pia anatazamiwa kuwa miongoni mwa wanaopewa nafasi ya kukinoa kikosi hicho.

Lopetegui amewahi kuinoa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Hispania na yuko katika msimu wake wa tatu na Sevilla, ambayo bado ana mkataba nayo hadi mwaka 2024.

# Ofa nne zatolewa kuinunua Chelsea

**LONDON,** England

KULIKUWA na ofa nne zilizothibitishwa kuinunua Chelsea kabla ya tarehe ya mwisho ya Ijumaa, kwa mujibu wa ripoti.

Chelsea inauzwa na Roman Abramovich, ambaye mali zake zimezuiliwa na serikali ya England na Umoja wa Ulaya (EU) kutokana na uvamizi wa Russia nchini Ukraine.

Abramovich anadaiwa kuiweka sokoni klabu hiyo aliyoinunua mwaka 2003, kwa pauni bilioni tatu.

Kampuni ya uwekezaji ya Raine Group inasimamia mchakato wa kuuza klabu hiyo, na fedha zozote zitaelekezwa kwa shirika la kutoa misaada au katika akaunti iliyofungiwa.

Mmiliki mpya wa Chelsea atalazimika kuidhinishwa na serikali na pia kupitisha ukaguzi wa kawaida wa Ligi Kuu England.

Mtu mwingine aliyetajwa kuwania nafasi ya kuinunua klabu hiyo ni Nick Candy.

Msemaji wa Candy anayemiliki Kampuni ya Blue Football Consortium alisema, kama ilivyoripotiwa na BBC Sport: "Ninaweza kuthibitisha makampuni mawili ya Korea Kusini, Hana Financial Group na C&P Sports Group ni sehemu muhimu ya muungano wa kimataifa wa wawekezaji wa Candy. Ushiriki wao ni mwakilishi wa Chelsea.

"Candy anataka kuendeleza upya Stamford Bridge iwapo atafanikiwa kuinunua klabu hiyo.



CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# TRA KUMWAGA BILIONI 1.6 UJENZI KITUO CHA MICHEZO

**Na Saada Akida**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imetenga Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Michezo kilichopo Kurasini jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Lengo la kujenga kituo hicho ni kuendeleza michezo lakini pia ni kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ambaye amedhamiria kurejesha heshima ya michezo ndani na nje ya nchi. Akizungumza na gazeti hili jijini katika bonanza la kuzipongeza timu za mamlaka hiyo, Naibu Kamishna Mkuu, Mcha Mcha, alisema TRA itaendelea kuunga mkono michezo kwa sababu ina umuhimu .

"Kwa mwaka huu tumeandaa Sh. bilioni 1.6 kwa ajili ya kujenga kituo hicho cha michezo lakini pamoja na kutenga fedha kwa ajili kusaidia timu hizo ili kuzisaidia zifanye vizuri katika mashindano mbalimbali," alisema Mcha.

Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa TRA, Peter Ntale alisema kituo hicho kitakuwa na uwanja wa michezo ya soka, netiboli, wavu, kikapu na vyumba vya kubadilisha nguo wachezaji.

Ntale alisema lengo la kujenga kituo hicho ni kuendeleza vipaji vya wafanyakazi wa TRA na mamlaka nyingine ambazo zitajitokeza kushiriki michuano mbalimbali itakayocheza kituoni hapo baada ya ujenzi kukamilika.

"Kituo hiki kitashirikisha michezo minne kwa ajili ya wachezaji kufanya mazoezi na mashindano tofauti, kwa hapa Dar es Salaam hii itatusaidia kupunguza gharama za kukodi uwanja, pia tuna mikakati ya kushiriki michuano nje ya nchi ili kujiongezea uwezo zaidi," alisema Ntale.

Mlezi wa wachezaji wa TRA ambaye ni Naibu Mkurugenzi wa Idara ya Fedha, Anna Mndeme, alisema baada ya kuwapo na changamoto ya muda mrefu sehemu ya kufanyia mazoezi, kukamilika kwa kituo hicho kutarahisisha na kutatua shida ya uwanja.

Makamu Mwenyekiti wa SHIMMUTA, Rosalyne Masama, aliishukuru TRA kwa kuendelea kudhamini michezo inayoandaliwa na shirikisho lao lakini pia aliwaomba waendelee kufanya hivyo kwa ajili ya kuendeleza michezo kwa wafanyakazi wote nchini.



Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mcha Hassan Mcha (watatu kutoka kushoto), akiwa na wachezaji wa timu mbalimbali za mamlaka hiyo zilizofanya vizuri katika mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma na Kampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) yaliyofanyika mwaka huu. TRA iliaandaa bonanza maalumu la kuwapongeza lililofanyika katika viwanja vya Gymkhana Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Serengeti Girls dimbani Botswana*

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), inatarajia kuvaana na wenyeji Botswana katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia U-17 itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Obed Itani Chilume ulioko katika mji wa Francistown nchini humo.

Serengeti Girls inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 7-0 waliopata katika mechi ya kwanza iliyochezwa nyumbani kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar Machi 6, mwaka huu.

Mshindi wa jumla wa mechi hiyo atakutana na Burundi ambayo ilisonga mbele baada ya wapinzani wake, Djibouti kujitoa.

Kocha Mkuu wa Serengeti Girls, Bakari Shime alisema kikosi chake kilifika salama Botswana na wachezaji wote wako fiti na tayari kwa mchezo huo.

Shime alisema wamejipanga kuendelea kupambana kusaka matokeo ya ushindi ili wasonge hatua inayofuata na hawatabweteka na ushindi walioupata nyumbani.

"Mechi ya kwanza tulipata ushindi mkubwa hii ni baada ya Botswana kufanya makosa, matokeo ya nyumbani yanatubeba kutocheza kwa presha kubwa lakini tunatakiwa tusibweteke na kufanya makosa yatakayotugharimu na kuwapa nafasi wapinzani wetu kushinda," alisema Shime.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 20/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1764 | CSKA Moscow vs Rubin Kazan | 1.40 | 4.44 | 7.10 |
| 14:30 | 2522 | Venezia vs Sampdoria | 2.64 | 3.29 | 2.64 |
| 15:00 | 3250 | Dundee FC vs Rangers | 9.63 | 5.31 | 1.28 |
| 15:00 | 4555 | Monaco vs Paris St Germain | 3.42 | 3.66 | 2.00 |
| 15:30 | 2619 | Crystal Palace vs Everton | 2.02 | 3.30 | 3.60 |
| 16:30 | 5341 | Sochi vs Kryliya Sovetov | 1.87 | 3.48 | 3.87 |
| 17:00 | 1872 | Lorient vs Strasbourg | 3.32 | 3.22 | 2.20 |
| 17:00 | 2208 | Empoli vs Verona | 2.65 | 3.45 | 2.55 |
| 17:00 | 3068 | Rennes vs Metz | 1.27 | 5.39 | 10.98 |
| 17:00 | 3407 | Angers vs Brest | 2.19 | 3.24 | 3.34 |
| 17:00 | 3789 | Bordeaux vs Montpellier | 2.43 | 3.39 | 2.79 |
| 17:00 | 4003 | Juventus vs Salernitana | 1.26 | 5.55 | 11.64 |
| 17:30 | 3958 | RB Leipzig vs Eintracht Frankfurt | 1.40 | 4.88 | 6.77 |
| 18:00 | 5320 | Mladost Lucani vs Metalac | 1.70 | 3.57 | 4.34 |
| 18:00 | 5564 | Southampton vs Manchester City | 7.65 | 4.92 | 1.35 |
| 18:15 | 1717 | Celta Vigo vs Betis | 2.24 | 3.39 | 3.14 |
| 18:15 | 5818 | Cadiz CF vs Villarreal | 4.40 | 3.60 | 1.80 |
| 18:30 | 1570 | Pacos Ferreira vs Moreirense | 2.25 | 3.15 | 3.20 |
| 18:30 | 4654 | Gil Vicente vs Maritimo | 1.80 | 3.40 | 4.43 |
| 18:30 | 4831 | Grasshoppers vs FC Basel | 2.91 | 3.55 | 2.23 |
| 18:30 | 5757 | FC Lugano vs Lausanne-Sport | 1.70 | 3.70 | 4.64 |
| 18:45 | 4305 | PSV Eindhoven vs Fortuna Sittard | 1.08 | 9.06 | 21.66 |
| 18:45 | 5836 | Vitesse Arnhem vs Waalwick | 1.60 | 3.86 | 5.08 |
| 19:00 | 2852 | Fenerbahce vs Konyaspor | 2.00 | 3.45 | 3.50 |
| 19:00 | 4936 | Genclerbirligi vs Kocaelispor | 1.97 | 3.28 | 3.48 |
| 19:05 | 4797 | Reims vs Lyon | 4.08 | 3.58 | 1.85 |
| 19:30 | 1154 | VfL Wolfsburg vs Bayer Leverkusen | 2.94 | 3.44 | 2.30 |
| 19:30 | 4420 | Tottenham vs West Ham | 1.72 | 3.96 | 4.41 |
| 20:00 | 1356 | Dinamo Moscow vs Rostov | 1.44 | 4.22 | 6.67 |
| 20:00 | 5575 | Roma vs Lazio | 2.49 | 3.39 | 2.74 |
| 20:15 | 3570 | Leganes vs Sporting Gijon | 2.22 | 3.03 | 3.33 |
| 20:30 | 1673 | Sevilla FC vs Real Sociedad | 2.07 | 3.25 | 3.70 |
| 20:30 | 3708 | KAA Gent vs Anderlecht | 2.29 | 3.29 | 2.99 |
| 20:30 | 4255 | Ujpest FC vs Budapest Honved | 2.07 | 3.36 | 3.12 |
| 20:30 | 5813 | Red Star Belgrade vs Kolubara | 1.01 | 19.19 | 38.38 |
| 21:00 | 3015 | CD Trofense vs GD Chaves | 3.18 | 3.03 | 2.27 |
| 21:00 | 3400 | Nottingham vs Liverpool | 9.81 | 5.88 | 1.25 |
| 21:00 | 5851 | Benfica vs GD Estoril | 1.32 | 5.12 | 8.26 |
| 21:30 | 2560 | FC Koln vs Borussia Dortmund | 3.29 | 3.74 | 2.02 |
| 22:00 | 3798 | Willem II Tilburg vs AZ Alkmaar | 5.29 | 4.02 | 1.56 |
| 22:00 | 4034 | Bodo Glimt vs Lillestrom | 1.51 | 4.12 | 5.18 |
| 22:00 | 5041 | Bragantino SP vs Palmeiras | 2.94 | 2.99 | 2.35 |
| 22:00 | 5361 | 9 De Octubre FC vs Gualaceo SC | 1.55 | 3.80 | 5.20 |
| 22:45 | 1930 | Bologna vs Atalanta | 4.19 | 3.74 | 1.81 |
| 22:45 | 2263 | Marseille vs Nice | 2.15 | 3.24 | 3.44 |
| 23:00 | 4202 | Real Madrid vs Barcelona | 2.20 | 3.49 | 3.15 |
| 23:00 | 4892 | Portimonense vs Sporting Braga | 4.05 | 3.36 | 1.89 |
| 23:00 | 5122 | St Truiden vs Kfco Wilrijk | 1.53 | 4.13 | 5.51 |
| 23:30 | 2114 | CD Palestino vs Colo Colo | 3.67 | 3.33 | 1.89 |
| 23:45 | 2688 | Boavista vs Porto | 7.00 | 4.80 | 1.42 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Machi 20, 2021

Nipashe




## Valverde afurahia kiwango cha Barca

HABARI UK 21



Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco (wa pili kulia), akifuatilia kwa makini mazoezi ya timu hiyo kwa ajili ya mechi ya Kundi D ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo mjini Cotonou nchini Benin. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga: Tumewazidi hapa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema kujituma kwa wachezaji katika kila mechi na ushirikiano wa viongozi ndani ya timu hiyo ni sababu ya wao kufanya vizuri kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inaendelea hapa nchini.

Yanga inaongoza ligi ikiwa na pointi 45 ikiwa hawajapoteza mechi yoyote kati ya michezo 17 waliyocheza na wako mbele kwa alama nane na Simba ambayo inashika nafasi ya pili ikiwa na point 37.

Nabi aliliambia gazeti hili umoja ulioko ndani ya klabu hiyo ambao pia unawahusisha wanachama na mashabiki unawaongezea nguvu wachezaji ambao wanapambana kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kocha huyo alisema benchi la ufundi likifanya kazi yake, wachezaji wakijitoa na kujituma kila mechi pamoja na viongozi kutekeleza vyema majukumu yao, ni wazi timu itavuna matokeo chanya katika kila mechi iliyopo mbele yao.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa na wachezaji wanatakiwa kujituma na kujitoa zaidi kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yetu, lakini pia viongozi watakiwa kushirikiana pamoja ili kufikia malengo," alisema Nabi.

Alisema ushirikiano na umoja ni silaha nzuri waliyonayo inayowafanya waendelee kuvuna pointi katika kila mechi na sasa wanatofautiana pointi nane na timu iliyoko katika nafasi ya pili.

Nabi alisema mechi zinazofuata zote ni ngumu lakini wameahidi kuendelea kupambana kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia malengo ya kutwaa ubingwa msimu huu.

# Simba yasaka rekodi mpya

## Yajipanga kutinga robo fainali ugenini kwa kuifunga Asec Mimosas lakini...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba watashuka kwenye Uwanja wa L'Amitie, Cotonou nchini Benin kuvaana na Asec Mimosas kutoka Ivory Coast katika mechi ya raundi ya tano ya michuano hiyo.

Simba ambayo iliwasili nchini humo salama Ijumaa na endapo itapata ushindi katika mechi hiyo, itafuzu moja kwa moja hatua inayofuata bila kujali matokeo ya mechi nyingine ya kundi hilo kwa sababu itafikisha pointi 10.

**Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara watamaliza hatua ya makundi nyumbani Aprili 3, mwaka huu kwa kuwakaribisha US Gendarmerie kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.**

Kocha Mkuu wa Simba Mhispania Pablo Franco alisema kikosi chake kinakabiliwa na mchezo mgumu na endapo watafanikiwa kupata ushindi, basi wataweka historia mpya ya kufuzu wakiwa kwenye ardhi ya ugenini.

"Ni mchezo ambao huenda ukatupa tiketi ya kufuzu robo fainali, hivyo natamani kuona wachezaji wangu wote wakiwa kwenye kiwango bora na wakipambana ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, lakini pia nikitarajia kutazamia wachezaji wengine ambao hawajacheza mechi nyingi na hawakuwa fiti kwa asilimia zote kama Denis Kibu, Thadeo Lwanga na Chris Mugalu kama wanaweza kurudi katika utimamu wao uliozoeleka," alisema Pablo.

Kocha huyo alisema wanahitaji kucheza kwa tahadhari kwa sababu wapinzani wao wanahitaji kushinda na kujiimarisha kwenye msimamo wa kundi hilo ambalo liko wazi kwa klabu zote nne.

Haitokuwa mechi rahisi kwa Simba kwani Asec Mimosas pamoja na kwamba si uwanja wake halisi wa nyumbani, lakini imeshinda mechi zake zote mbili dhidi ya RS Berkane mabao 3-1 na US Gendarmerie mabao 2-1 na hilo lilithibishwa na Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally.

"Kwao utakuwa mchezo muhimu zaidi, kwa sababu ni wa mwisho kucheza nyumbani, baada ya hapo watawafuata RS Berkane na US Gendarmerie, lakini pia imeonekana timu hiyo inakuwa hatari zaidi inapocheza kwenye uwanja huo kwa sababu imeshinda mechi zote mbili, lakini sisi tuko kwenye kampeni ya kushinda ugenini, kwani safari hii tunataka kufuzu robo fainali tukiwa kwenye ardhi ya ugenini, siku zote Simba hushinda mechi ngumu na kuishangaza Afrika," alisema meneja huyo.

Asec Mimosas inacheza mechi zake nchini Benin, kutokana na viwanja vyenye sifa vilivyoko Ivory Coast kuwa kwenye ukarabati wa maandalizi kwa ajili ya fainali za mwakani za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), na kwa maana hiyo uwanja utakaotumika leo hautakuwa mgeni kwa baadhi ya wachezaji wa Simba akiwamo Aishi Manula, Kibu, Mohamed Hussein na Israel Mwenda ambao waliuchezea Oktoba 10, mwaka jana wakiwa na Timu ya Taifa ( Taifa Stars) na kushinda bao 1-0.

Simba inaongoza Kundi D ikiwa na pointi saba ikifuatiwa na Asec Mimosas yenye pointi sita sawa na RS Berkane ya Morocco wakati US Gendarmerie ya Niger yenye pointi nne ikishika mkia.



9 770856 541002